# Tazama Yuaja

## *Kuhusu Toleo Hili.*

Kuna makanisa mengi duniani yanayo dai kuwa yanafundisha ukweli. Yote pia yana mafundisho tofauti yaliyo mafundisho na desturi ya watu.

Muungano wa makanisa na uwongozi wa makanisa binafsi yamefanya kazi miaka mingi kuunganisha makanisa yote kwa mafundisho yaliyofanana. Hadi sasa, lengo hili halijafikiwa kika-milifu.

Mpenzi msomaji, kijitabu hiki kimeandaliwa kukusaidia kufanya uamuzi bora wa maisha haya, ili kujiandaa kwa maisha ya milele yanayoanza hivi karibuni Bwana wetu Yesu ajapo. Kwa maelezo zaidi, tuandikie kwa kutumia an-wani iliyoko nyuma ya jarida hili.


## *Umuhimu wa Mafundisho ya Biblia*

Bibilia yenyewe inadhibitisho takatifu ya mahali ilikotoka. Hakuna kitabu kingine kinachoweza kujibu maswali ya ubongo, au kutosheleza mahitaji ya moyo kama vile bibilia. Inatosheleza umri zote na masharti ya maisha, na imejaa mawaidha ya maisha na mwangaza inayotakasa moyo. Katika Bibilia mna ufunuo wa Mungu aliye hai. Tukimpokea kwa imani, ana nguvu ya kubadilisha maisha yetu.

Bibilia, katika historia yake yote, mkono mtakatifu umekuwa ukiifunika, na kuutunza kwa ajili ya walimwengu.

Ndipo ulimwengu ikipokea ujumbe huo pia ikijiandaa kwa ujumbe wa mwisho kwa mwanadamu, wa kuumaliza utawala wa dhambi na kuja mara ya pili kwa Bwana katika utukufu. "tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapofika." Matayo 24:14.

Kama kiongozi, Bibilia haina pingamizi. Yakupa amani tulivu kwa aaminiye na tumaini yenye msingi kwa mambo yajayo. Inatatua mambo magumu ya maisha, na mwisho wake na kukupa mutisha wa maisha safi, uvumilivu, na matendo mema. Yajaza moyo na upendo wa Mungu na matamanio ya kuwatenda wengine mambo yaliyo mema, hivyo kukuandaa kutumika hapa na makao ya milele ya mbinguni. Yafundisha umuhimu wa moyo kwa kufunua gharama iliyolipwa kuukomboa. Yafunua njia pekee ya kutoka kwa dhambi na, mawaidha ya kipekee ya maisha yaliyowahi kutolewa.



"Tazama yuaja na mawingu; na kila jicho litamwona" Ufunuo I:7

**Maandiko yote yatufaa nini?**

"Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki." 2 Timotheo 3:16.

**Nini lengo la Mungu kwa kutupa maandiko?**

"Ili mtu wa Mungu awe kamilil, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema." Fungu la 17.

**Nani aliye waongoza waliyonena?**

"Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu." 2 Petro 1:21.

**Kwa kusudi gani maandiko yaliandikwa?**

"Kwa kuwa yote yaliyotangulia kuandikwa yaliandikwa ili kutufundisha sisi; ili kwa saburi na faraja ya maandiko tupate kuwa na tumaini." Warumi 15:4.

**Kristo alisema nini kuhusu mafundisho ya maandiko?**

"Mwayachunguza maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia." Yohana 5: 39.

**Imani ya isaya ilikuwa na msingi upi katika neno la Mungu?**

"Majani yakauka, ua lanyauka; Bali neno la Mungu wetu litasimama milele." Isaya 40:8.

**Baraka zipi kuu kristo aliwapa wanafunzi wake katika ufufuo wake?**

"Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko." Luka 24:45.

## *Nguvu katika neno la Mungu.*

**Kristo aliwakemeaje waliokuwa na maandiko lakini hawakufahamu?**

"Yesu akajibu, akawaambia, Mwapotea, kwa kuwa hamyajui maandiko wala uweza wa Mungu." Mathayo 22:29.

**Nani Kristo alitamka kuwa amebarikiwa?**

"Lakini yeye alisema, Afadhali, heri walisikao neno la Mungu na kulishika." Luka 11:28.

**Ni ibada ya namna gani hutokea baada ya mafundisho ya uwongo?**

"Nao waniabudu bure, Wakifundisha mafundisho Yaliyo maagizo ya wanadamu." Mathayo 15:9.

**Katika mafundisho yapi wengi watapotea siku za mwisho?**

"Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani." 1 Timotheo 4: 1. Tazama 2 Petro 2:1.

**Wanadu watageuza masikio yao wapi?**

"Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; Nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo." 2 Timotheo 4:3-4.

**Tunawezaje kuamua ukweli wa kila fundisho?**

"Jaribuni mambo yote; lishikeni lililo jema." I Wathesalonike 5:21.

**Maandiko yanaweza kumfanyia nini yeye anaye yaamini?**

"Na yakuwa tangu ututoni umeyajua maandiko matakatifu, ambayo yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu kwa imani iliyo katika Kristo Yesu ." 2 Timotheo 3:15.

**Ni kwa njia gani watatakaswa?**

"Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli." Yohana 17:17.

**Wanafunzi wa Yesu ni akina nani, na ni kazi gani ya neema ukweli unawafanyia wale wanaoupokea?**

"Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli; tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru." Yohana 8:31-32.

**Asili ya neno la mungu ni nini?**

"Maana neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko

upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatamua mawazo na makusudi ya moyo." Waebrania 4:12.

**Ni kwa nini waamini hutakaswa?**

"Ninyi mmekwisha kuwa safi kwa sababu ya lile neno nililowaambia." Yohana 15:3.

**Kwa njia gani kijana aitakase njia yake?**

"Jinsi gani kijana aisafishe njia yake? Kwa kutii, kulifuata neno lake." Zaburi 119:9.

## *Umhimu wa Maombi*

**Neno gani la heshima ambalo mwandishi wa Zaburi anatumia kuongea na Mungu?**

"Wewe usikiaye kuomba, wote wenye mwili watakujia." Zaburi 65:2.

**Ni kwa masharti gani Zaburi inasema Mungu hatajibu maombi?**

"Kama ningaliwaza maovu moyoni mwengu, Bwana asingesikia." Zaburi 66:18. Tazama Isaya 59:1-2; Yakobo 4:3.

**Maombi ya Suleimani asema ni chukizo?**

"Yeye aligeuzaye sikio lake asiisikie sheria, hata sala yake ni chukizo." Mithali 28:9.

**Yesu alitufundisha kuwaombea nani?**

"Lakini mimi nawaambia, wapendeni adui zenu waombeeni wanaowaudhi." Mathayo 5:44.

**Kwa njia gani twaweza kuepuka majaribu?**

"Kesheni, mwombe, msije mkaingia majaribuni; roho i radhi, lakini mwili ni dhaifu." Mathayo 26:41.

**Mtu ataulizaje ili apokee?**

"Illa naomba kwa imani, pasipo shaka yo yote; maana mwenye shaka ni kama wimbi la bahari lililochukuliwa na upepo, na kupeperushwa huku na huku. Maana mtu kama yule asidhani ya kuwa atapokea kitu kwa Bwana." Yakobo 1:6-7. Tazama Marko 11:24.

**Fahamu**-Maombi ni ufunguo mikononi mwa mwenye imani kufungua hazina zote za mbingu mahali palipo utajiri usio na kifani wa Mungu.

**Tunasihiwa tukeshe kwa nini?**

"Lakini mwisho wa mambo yote umekaribia; basi iweni na akili, mkeshe katika sala." I Petro 4:7.

**Tuombe mara ngapi?**

"Ombeni bila kukoma." I Wathesolonike 5:17. "mkisubiri katika kusali, mkidumu." Warumi 12:12.

**Ni kwa masharti gani tumeahidiwa mibaraka tunayohitaji?**

**"Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa; kwa maana kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona; naye abishaye atafuguilwa." Mathayo 7:7-8.**

**Fahamu-Maombi ni ufunguaji wa moyo kwa Mungu kama kwa rafiki. Maombi hayabadilishi Mungu; lakini sisi hubadilika na uhusiano wetu kwa Mungu. Yanatuweka katika mfereji wa mibaraka, na katika sura ya mawazo ambayo Mungu anaweza kutupatia mahitaji yetu mfululizo na kwa usalama.**

## *Uumbaji na Muumbaji*

**Ni kutokana na nani Mbingu na Inchi ziliumbwa?**

"Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi." Mwanzo 1:1.

**Kwa jinsi gani Mungu alifanya Mbingu na Nchi kuishi?**

"Kwa neno la Bwana mbingu zilifanyika, Na jeshi lake lote kwa punzi ya kinywa chake.... Maana Yeye alisema, ikawa; Na Yeye aliamuru, ikasimama." Zaburi 33:6-9.

**Kupitia kwa nani Mungu aliumba vitu vyote?**

"Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbingu na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana; ikiwa ni vitu vya enzi au usultani au enzi au mamlaka; vitu vyote viliumbwa kwa njia yake, na kwa ajili yake." Wakolosai 1:16. Tazama Waebrania 1:1-2.

**Ni chombo kipi Mungu alikitumia kwa kuiumba nchi?**

"Maana Bwana aliyeziumba mbingu, asema hivi; yeye ni Mungu ndiye aliyeumba dunia na kuifanya, ndiye aliyeifanya imara; hakuiumba ukiwa, aliiumba ili ikaliwe na watu; mimi ni Bwana, wala hapana mwingine." Isaya 45:18.

**Kwa jinsi gani Mungu alipatia wakaaji nchi aliyoiumba?**

"Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai....." Mwanzo 2:7.

**Ni kwa mfano wa nani mwanadamu aliumbwa?**

"Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba mwanamume na mwanamke." Mwanzo 1:27.

**Je, Kilakitu kiliumbwa na Kristo?**

"Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana; ikiwa ni vitu vya enzi, au usultani, au enzi, au mamlaka; vitu vyote viliumbwa kwa njia yake, na kwa ajili yake: Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu ili kwamba awe mtangulizi katika yote." Wakolosai 1:16-18.

**Ni maandiko gani tunasoma wazi wazi kwamba ni nguvuza uumbaji ndizo zinazowabadilisha waaomini?**

"Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliitengeneza ili tuenende nayo." Waefeso 2:10.

## *Mwanzo wa Dhambi*

**Ni kwa jinsi gani vita baina ya Yesu na shetani vinavyosimuliwa?**

"Kulikuwa na vita mbinguni mikaeli na malaika zake wa kapigana na yule joka, yule joka naye akapigana nao pamoja na malaika zake; nao hawakushinda, wala mahali pao hapakuonekana tena mbinguni. Yule joka akatupwa yule mkubwa, nyoka wa zamani aitwae ibilisi na shetani, audanganyaye ulim-wengu wote; akatupwa hata nchi, na malaika zake wakatupwa pamoja naye." Ufunuo 12:7-9.

**Fahamu**-Vita hivi vilianza huko mbinguni na vinaendelea hapa ulimwenguni."

**Dhambi zilianzia kwa nani?**

"Atendaye dhambi ni wa Ibilisi; kwa kuwa Ibilisi hutenda dhambi tangu mwanzo." 1 Yohana 3:8.

**Tangu wakati gani shetani amekuwa muuaji?**

"Ninyi ni wa baba yenu Ibilisi, na tamaa za baba yenu ndizo mpendazo kuzitenda, yeye alikuwa muuaji tangu mwanzo, wala hakusimama katika kweli, kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yake...." Yohana 8:44.

**Shetani alikuwa mwenye dhambi?**

"Ulikuwa mkamilifu katika njia zako tangu siku ile ulipoumbwa, hata uovu ulipoonekana ndani yako." Ezekieli 28:15.

Hii na maandishi mengine katika yohana 8:44, kwa kuwa "hamna hiyo kweli ndani yake," yanaonyesha kwamba shetani alikuwa mkamilifu na mwenye ukweli. Petro anaongea juu ya malaika waliotenda dhambi." (tazama 2 Peter 2:4) na yudas anamwita "malaika mwenye hakuhifadhi njia zake za kwanza." Yuda 6. Pale mwanzo walikuwa bila dhambi.

**Ni maandiko ya Kristo yanayoonyesha jukumu la mwanzo wa dhambi kuwa la shetani na malaika wake?**

"Kisha atawaambia na wale walioko mkono wake wa kushoto, Ondokeni mliolaaniwa mwende katika moto wa milele, alioekewa tayari Ibilisi na malaika zake." Mathayo 25:41.

## *Kuanguka kwa Mwanadamu*

**Ni lini dhambi na mauti iliingia duniani?**

"Kwa hiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi [Adam] iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi." Warumi 5:12.

**Ni kwa maneno gani Mungu anamhukumu Caini kuwa mwenye dhambi?**

Akasema, Umefanya nini? Sauti ya damu ya ndugu yako inanililia kutoka katika ardhi. Basi sasa, umelaaniwa wewe katika ardhi." Mwanzo 4:7-11.

**Ni laana gani iliyoongezewa kwa sababu ya mauaji ya kwanza?**

"Bwana akamwambia Kaini,.... Basi sasa, umelaaniwa wewe katika ardhi, iliyofumbua kinywa chake ipokee damu ya ndugu yako kwa mkono wako; Utakapoilima ardhi haitakupa mazao yake; utakuwa mtoro na mtu asiye na kikao." Mwanzo 4:9-12.

**Ni jinsi gani dunia na hata mimea vilivyoadhiliwa na dhambi za Adamu?**

"Kwa uchungu utakula mazao

yake siku zote za maisha yako; michomgoma na miiba itakuzalia, naye utakula mboga za kondeni." Mwanzo 3:17-18.

**Ni nini mshahara wa dhambi?**

"Mshahara wa dhambi ni mauti." Warumi 6:23. "Kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika." Mwanzo 2:17. "Roho ile itendayo dhambi itakufa." Ezekieli 18:4.

**Dhambi inajulikana kama nini?**

"Kila atendaye dhambi, afanya uasi; kwa kuwa dhambi ni uasi." 1 Yohana 3:4.

**Ni nini kinafuata dhambi?**

"Halafu ile tamaa ikiisha kuchukua mimba huzaa dhambi." Yakobo 1:15.

"Na kila tendo lisilotoka katika imani ni dhambi." Warumi 14:23.

**Fahamu**-Tunaasi Mungu tukikosa uaminifu au imani kwake.

## *Matokeo ya Dhambi*

**Ni nini matokeo ya mwisho au tunda la dhambi?**

"Na ile dhambi ikiisha kukomaa huzaa mauti." Yakobo 1:15.

**Ni jinsi gani mwanadamu ataweza kuiepuka malipo hayo?**

"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu." Warumi 6:23.

## *Thambi Ni Nini*

**Ni nini matokeo ya dhambi ya kutokujali?**

"Maana kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi, bali kuna kuitazamia hukumu yenye kutisha, na ukali wa moto ulio tayari kuwala wao wapingao." Waebrania 10:27-29.

## *Sheria ya Mungu*

**Ni jinsi gani Mungu aiitangaza sheria yake kwa watu wake?**

"Na Mungu akanena nanyi kutoka katikati ya moto; mkaisikia sauti, lakini hamkuona umbo lolote. Akawahubiria agano lake, alilowaamuru kulitenda." Kumbukumbu 4:12-13. Tazama pia Nehemia 9:13-14. Amri kumi tazama. Kutoka 20:2-17.

**Zinafahamika vipi hizi sheria?**

"Mche Mungu, nawe uzishike amri zake, Maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu." Mhubiri 12:13.

**Asili ya sheria ya Mungu ni gani?**

"Na ile amri ni takatifu, na ya haki, na njema... kusudi kwa ile amri dhambi ilizidi kuwa mbaya mno." Warumi 7:12,14.

**Mtu ataweza kumjua Mungu na akose kuzitii sheria zake?**

"Yeye asemaye, nimemjua, wala hazishiki amri zake ni mwongo wala kweli haimo ndani yake." I Yohana 2:4.

**Tutaweza kujua kama tunawapenda wenzetu?**

"Kwa haya tunajua tunawapenda wana wa Mungu, tunapo mpenda mungu na kuziweka amri zake." I Yohana 5:2.

**Ni nini upendo wa Mungu?**

"Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake." Fungu la.3

**Ni vipi kristo alivyo hudumia amri za baba?**

"Mkizishika amri zangu, mtakaa katika pendo lamgu; kama vile nilivyozishika amri za Baba yangu na kukaa katika pendo lake." Yohana 15:10.

**Kama mtu anakiri kuwa yuko ndani ya Yesu, ni vipi anatakiwa kutembea?**

"Yeye asemaye kuwa anakaa ndani yake inampasa kuenenda mwenyewe vile vile kama yeye alivyoenenda." I Yohana 2:6.

**Ni vipi Yesu alivyoelezea sheria za baba yake?**

"Msidhani yakuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la sikuja kutangua bali kutimiliza." Mathayo 5:17.

**Ni nini alifundisha kulangana na uthabiti wa sheria?**

"Kwa maana amini nawaambia, mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yadi moja wala nukta moja ya torati haitaoondoka hata yote yatimie." Fungu la 18.

**Ni vipi Mungu anahusika na tabia za wakristo?**

"Maana mtu awaye yote atakayeshika sheria yote ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote." Yakobo 2:10-12.

## *Sheria na Injili*

**Ni nini kusudi ya sheria?**

"Kwa sababu hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki mbele zake kwa matendo ya sheria; kwa maana kutambua dhambi huja kwa njia ya sheria." Warumi 3:20.

**Ni nini injili imepitishwa kuwa?**

"Kwa maana sionei haya injili, kwa sababu ni uweza wa Mungu uletao wokovu, kwa kila aaminiye." Warumi 1:16.

**Nini inaonyesha kuwa amri kumi zilizosemwa na kuandikwa katika mlima wa Sinai ni amri ya uhuru kwa wakristo?**

**"Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote ila akajikwaa, katika neno moja; amekosa juu ya yote kwa maana yeye aliyesema, usizini pia alisema, Usiue. Basi ijapokuwa hukuzini, lakini umeua, umekuwa mvunja sheria. Semeni ninyi, na kutenda kama watu watakaohukumiwa kwa sheria ya uhuru." Yakobo 2:10-12.**

**Yesu anatoa ahadi gani kuhusu agano jipya?**

"Lakini sasa amepata huduma iliyo bora zaidi, kwa kadiri alivyo mjumbe wa agano lililo bora, lililoamriwa juu ya ahadi zilizo bora....Maana hili ndilo agano nitakaloagana na nyumba ya Israeli Baada ya siku zile, asema Bwana; Nitawapa sheria zangu katika nia zao, Nakatika mioyo yao nitaziandika." Waebrania 8:6,10.

**Kwa nini mafikira ya tamaa ya mwili ni adui wa Mungu?**

"Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kutii." Warumi 8:7.

**Binadamu mwenyewe bila msaada kutoka kwa Mungu ataweza kutunza sheria?**

"Mimi ni mzabibu; nanyi ni matawi, akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote." Yohana 15:5. Pia tazama Warumi 7:14-19.

**Ni nani alisema ataingia ufalme wa mbinguni?**

"Si kila mtu aniambiaye, Bwana Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyae mapenzi ya baba yangu aliye mbinguni." Math-ayo 7:21.

**Ni vipi mwanadamu ataweka kipimo kulingana na sheria za Mungu?**

"Basi mtu yeyote atakayevunja amri moja katika hizi zilizo ndogo, na kuwafundisha watu hivyo ataitwa mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni; bali mtu atakayezitenda na kuzifundisha, huyo ataitwa mkubwa katika ufalme wa mbinguni." Mathayo 5:19.

**Mwamini anatarajiwa kuendelea na dhambi baada ya hii?**

"Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi, ili neema izidi kuwa nyinyi? Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi?" Warumi 6:1-2.

**Ni kifungo kipi ambacho kinakata matumaini yote yakutakaswa kwa kazi?**

"Kwa sababu hakuna mwenye mwili atakayehesebiwa haki mbele zake kwa matendo ya sheria." Warumi 3:20.

**Ni kwa njia gani waomini wote katika Yesu wanahesabiwa haki?**

"Wanahesabiwa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika kristo Yesu." Fungu la 24.

**Yesu alitafsiri vipi kwa utakatifu sheria ya sita na ya saba?**

"Mmesikia watu wa kale walivyoambiwa, usiue, na mtu akiua, itampasa hukumu. Bali mimi nawaambieni, Kila amwoneaye ndugu yake hasira itampasa hukumu." Mathayo 5:21-22. Mmesikia kwamba imenenwa, Usuzini; lakini mimi nawaambia, kila mtu atazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake." Fungu la 27-28.

## *Mateso ya Yesu*

**Manabii walisema nini Yesu aliitwa kuvumilia?**

"Alionewa lakini alinyenyekea, wala hakufunua kinywa chake; kama mwana kondoo apelekwae machinjoni, Na kama vile kondoo anyamazavyo mbele yao wakatao manyoa yake; naam, hakufunua kinywa chake.Kwa kuonewa na kuhukumiwa aliondolewa; na maisha yake ni nani atakayeisimulia? maana amekataliwa mbali na nchi ya walio hai; alipigwa kwa sababu ya makosa ya watu wangu." Isaya 53:7-8.

**Yesu aliyajua mateso aliyokua anaenda kuyapata kabla ya kuyapata?**

"Akawachukua wale theneshara, akawaambia, tazameni, tunapanda

kwenda Yerusalemu, na mambo yote yatatimizwa, mwana wa Adamu aliyoandikiwa na manabii.Kwa kuwa atatiwa mikononi mwa mataifa, atafanyiwa dhihaka; atatendwa jeuri, na kutemewa mate; nao watampiga mijeledi, kisha watamwua." Luka 18:31-33.

**Ni mateso gani ya aibu Yesu alipata kutoka kwa wale askari?**

"Wakasokota taji ya miiba, wakaiweka juu ya kichwa chake, na mwanzi katika mkono wake wa kuume;wakapiga magoti mbele yake, wakamdhihaki, wakisema, salamu, mfalme wa Wayahudi! Kisha wakamtemea mate, wakautwaa ule mwanzi, wakampigapiga kichwani." Mathayo 27:29-30.

**Akiwa amefikishwa mahali pa kusulubishwa Yesu alipewa kinywaji kipi ili akili zake zipotee?**

"Wakampa kunywa divai iliyochanganyika na nyongo; lakini yeye alipoionja hakutaka kunywa." Mathayo 27:34.

**Ni katika maombi gani ya wale waliomsulubisha Yesu alliweza kuonyesha ukweli wa injili - upendo kwa wenye dhambi?**

"Na Yesu akasema, Baba uwasamehe kwani hawalijui walitendalo." Luka 23:34.

**Ni kwa maneno yapi Makuhani na wengine walimdhihaki Yesu naye?**

"Kadhalika na wale wakuu wa makuhani wakamdhihaki pamoja na waandishi na wazee, wakisema, 'Aliokoa wengine, hawezi kujiokoa mwenyewe. Yeye ni Mfalme wa Israeli; na ashuke sasa msalabani, nasi tutamwamini." Mathayo 27:41-42.

**Ni nini ilifunga tazamo hilo la kuogofya?**

"Basi Yesu alipokwisha kuipokea ile siki, alisema, imekwisha. Akainama kichwa akaisalimu roho yake." Yohana 19:30.

## *Kufufuka kwa Yesu*

"Na aliye hai; nami nalikuwa nimekufa, nazama, nihai milele na milele. Nami ninazo funguo za mauti na za kuzimu." Ufunuo 1:18

**Baada ya kufufuka ni madhara gani utabiri ulileltwa kwa wanafunzi wake?**

"Basi alipo fufuka katika wafu, wanafunzi wake wakakumbuka ya kuwa alisema hivi, wakaliamini lile andiko na lile neno alilolinena Yesu." Yohana 2:22.

"Kwa maana naliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi mwenyewe, ya kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko." I Wakorintho 15:3-4,

## *Kuhesabiwa Haki kwa Imani*

**Ni vipi Mungu anahesabia mwana damu haki?**

"Ili tukihesabiwa haki kwa neema yake, tupate kufanywa warithi wa uzima wa milele, kama lilivyo tumaini letu." Tito 3:7.

**Ni kwa njia gani kuhesabiwa haki kwa neema inapatikana kwa dhambi?**

"Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake, tutaokolewa na gadhabu kwa yeye." Warumi 5:9.

**Kuhesabiwa haki basi ni nini?**

"Basi, twaona ya kuwa mwanadamu huhesabiwa haki kwa imani pasipo matendo ya sheria." Warumi 3:28.

**Ni kwa njia gani pekee wenye dhambi wataweza kuhesabiwa haki au kutakaswa?**

"Hali tukijua yakuwa mwanadamu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria, bali kwa imani ya Kristo Yesu; sisi tulimwamini kristo Yesu ili tuhesabiwe haki kwa imani ya Kristo, wala si kwa matendo ya sheria;maana kwa matendo ya sheria hakuna mwenye mwili atakaye hesabiwa haki." Wagalatia 2:16.

**Ni katika msingi gani ambapo hakuna uwezo kuhesabiwa haki kwa mwenye dhambi?**

"Kwa sababu hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki mbele zake kwa matendo ya sheria; kwa maana kutambua dhambi huja kwa njia ya sheria." Warumi 3:20

**Kifo cha Yesu chashuhudia haya vipi?**

"Siibatili neema ya Mungu; maana, ikiwa haki hupatikana kwa njia ya sheria, basi Kristo alikufa bure." Wagalatia 2:21.

**Ni nini inasujudiwa kutokana na jaribio la kuhesabiwa haki kwa sheria?**

"Mmetengwa na Kristo, ninyi mtakao kuhesabiwa haki kwa sheria, mmeanguka na kutoka katika hali ya neema." Wagalatia 5:4.

**Kwa nini waisraeli hawakuufikia utakatifu?**

"Bali israeli wakiifuata sheria ya haki hawakuifikilia ile sheria. Kwa sababu gani? Kwa sababu hawakuifuata kwa njia ya imani, bali kana kwamba njia ya matendo.Wakajikwaa juu ya jiwe lile likwazalo." Warumi 9:31-32.

**Ni nini inathihirishwa na sheria?**

"Kwa maana kutambua dhambi huja kwa njia ya sheria." Warumi 3:20.

**Ni nini inaonyesha ukweli wa utakatifu ambao unapatikana kwa imani kusipokuwa na matendo ya sheria?**

"Lakini sasa haki ya Mungu imedhihirika pasipo sheria, inashuhudiwa na matorati na manabii." Warumi 3:21.

**Imani ina umuhimu upi?**

"Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza." Waebrania 11:6.

**Ni maandiko yapi yanaonyesha kuwa utakatifu ambao umepokewa kwa neema kupita kwa imani hautakiwi kutolewa udhuru kwa kuendelea kutenda dhambi?**

"Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi?" Warumi 6:1-2.

**Imani inaweza kutupilia mbali sheria za Mungu?**

Basi, je? twaibatilisha sheria kwa imani hiyo? Hasha! kinyume cha hayo twaithibitisha sheria." Warumi 3:31.

## *Kutubu*

**Ni akina nani wanaitwa watubu?**

"Si kuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi, wapate kutubu." Luka 5:32.

**Ni wangapi wenye dhambi?**

"Kwa maana tumekwisha kuwa shitaki wayahudi na wayunani wamekutwa chini ya dhambi." Warumi 3:9.

**Ni maombi yapi yanoyofaa kwa watenda dhambi?**

"Tutendeje, ndugu zetu?" "Yanipasa nifanye nini ili nipate kuokoka?" Matendo 2:37,16: 30.

**Ni majibu yapi yanayotarajiwa kutokana na maswali yao?**

"Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina la Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu." "Mwamini Bwana Yesu nawe utaokoka." Matendo 2:38,16 :31.

**Matokeo ya huruma ya mungu ni yapi?**

"Maana huzuni iliyo kwa jinsi ya Mungu hufanya toba liletalo wokovu." 2 Wakorintho 7:10.

**Yohana mbatizaji aliwasemea nini wafarisayo (saducess) alipowaona wakija mahali alikuwa anabatiza?**

"Enyi wazao wa nyoka, ni nani aliewaonya ninyi kuikimbia hasira itakayokuja?" Mathayo 3:7.

**Ni nini aliwaambia wafanye?**

"Basi zaeni matunda yapasayo toba." Fungu la 8.

## *Kuungama na Kusamehewa*

**Ni ahadi gani ambayo imetolewa kwa wale waungamao dhambi zao?**

"Tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutosafisha na udhalimu wetu." 1 Yohana 1:9.

**Ni matokeo yapi tofauti yanayokuja na pia kuungama dhambi?**

"Aifichaye dhambi zake hatafanikiwa, bali yeye aziungamaye na kuziacha atapata rehema." Methali 28:13.

**Ni nini Mungu ako tayari kufanya kwa wale wote wanatafuta msamaha?**

"Kwa maana wewe, Bwana u mwema, umekuwa tayari kusamehe, na mwingi wa fadhili kwa watu wote wakuitao." Zaburi 86:5.

**Ni kwa nani Daudi aliweka tumaini lake la msamaha?**

"Ee Mungu, unirehemu, sawasawa na fadhili zako. Kiasi cha wingi wa rahema zako, Ufute makosa yangu." Zaburi 51:1.

**Wakati Daudi alitubu dhambi zake ni nini alisema Mungu amefanya?**

“Nalikujulisha dhambi yangu, Wala sikuuficha upotovu wangu. Nalisema, Nitayakiri maasi yangu kwa Bwana, Nawe ukanisamehe upotovu wa dhambi yangu.” Zaburi 32:5.

**Ni onyo lipi ambalo lililotolewa kwetu na Mungu kwa sababu ametusamehe?**

“Tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyo wasamehe ninyi.” Waefeso 4:32.

**Ni kupita kwa nani kuungama na kusamehewa kunatolewa?**

“Mungu wa baba zetu alimfufua Yesu, ambaye ninyi mlimwua mkimtundika katika mti. Mtu huyo Mungu amemtukuza kwa mkono wake wakume awe mkuu na mwokozi, awape Waisraeli toba na msamaha wa dhambi.” Matendo 5:30-31.

## *Roho Mtakatifu na Kazi Yake*

**Ni ahadi gani ya thamani ambayo Yesu alitoa kwa wanfunzi wake mda mchache kabla ya kusulubishwa?**

“Nami nita mwomba baba, naye atawapa msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele.” Yohana 14:16.

**Ni jinsi gani ilikuwa muhimu kwa Yesu kwenda mabli?**

“Lakini mimi nawaambia iliyo kweli, yawafaa ninyi mimi niondoke, kwa maana mimi nisipoondoka, huyo msaidizi hatakuja kwenu; bali mimi nikienda zangu nitampeleka kwenu.” Yohana 16:7.

**Ni nani mfariji na nini alihitajika kufanya?**

“Lakini huyo msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia.” Yohana 14:26.

**Ni kazi gani nyingine mfariji alikuwa afanye?**

“Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha (halisi, ‘sadiki’) ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu.” Yohana 16:8.

**Ni kwa maneno yapi mfariji anaonyesha?**

“Lakini ajapo huyo msaidizi, nitakayewapelekea kutoka kwa baba, huyo Roho wa kweli atokaye kwa baba, yeye atanishuhudia.” Yohana 15:26.

**Ni nini Yesu Alisema Roho wa ukweli atafanya?**

“Lakini yeye atakapokuja, huyo roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake.” Yohana 16:13.

**Ni onyo gani basi linalotolewa?**

“Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitlwa muhuri hata siku ya ukombozi.” Waefeso 4:30.

**Ni nini Daudi aliombea?**

“Usinitenge na uso wako, wala roho yako mtakatifu usiniondolee.” Zaburi 51:11.

**Ni nani alitembea juu ya manabii kuwapatia ujumbe?**

“Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.” 2 Petero 1:21.

**Matokeo ya roho ni yapi?**

“Lakini tunda la roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi.” Wagalatia 5:22-23.

**Ni kutokana somo lipi tutaweza kujifunza?**

“Basi, ndugu zangu, kwa habari ya karama za roho, sitaki mkose fahamu.” 1 Wakorintho 12:1.

**Ni vipawa vipi vimepeanwa?**

“Na Mungu ameweka wengine katika kanisa, wa kwanza mitume, wa miujiza, kisha karama za kuponya wagonjwa, na masaidiano, na maongozi, na aina za lugha.” I Wakorintho 12: 28.

## *Ubatizo wa Mkristo*

**Ni sheria ipi inayolingana kwa ukaribu na kuamini injili?**

“Akawaambia, enededi ulimweguni mwote, mkaihubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiye amini, ataukumiwa.” Marko 16:15-16.

**Ni vipi watu walipokea mahubiri ya yohana?**

“Ndipo walipomwendea Yerusalemu, na uyahudi wote, na nchi zote za kandokando ya Yorodani; naye akawabatiza katika mto wa Yorodani, huku wakiziungama dhambi zao.” Mathayo 3:5-6.

**Mtume yakobo alilinganisha ubatizo katika maonyo yake katika siku hii kuu ya roho mtakatifu?**

“Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu.” Matendo 2:38.

**Kwa uhusiano wa ubatizo wa mkristo, ni nini inasafishwa?**

“Basi sasa, unakawilia nini? Simama, ubatizwe, ukaoshwe dhambi zako, ukiliita jina lake.” Matendo 22:16. Tazama Tito 3:5; 1 Petro 3:12.

**Ni kwa njia ipi dhambi zinaondolewa?**

“Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu yake.” Ufunuo 1:5.

**Waomini wanapobatizwa kwa Yesu ni nani wana mvaa?**

“Maana ninyi nyote mlibatizwa katika Kristo, wamemvaa Kristo.” Wagalatia 3:27.

**Ni kwa jinsi gani wale waliobatizwa, wamebatizwa ndani ya Yesu?**

“Hamfahamu yakuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake?” Warumi 6:3.

**Ni jinsi gani kubatizwa huku kumeelezewa?**

“Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.” Fungu la 4.

**Ni vipi basi tumeunganishwa na Yesu kutokana na kufa na kufufuka kwake?**

“Kwa maana kama tulivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika tutaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake.” Fungu la 5.

**Ni swali lipi towashi aliuliza baada ya philipo almuhubiria juu ya yesu?**

“Wakawa wakiendelea njiani, wakafika mahali penye maji; yule towashi akasema, tazama, maji haya; ni nini kinachonizuia nisibatizwe?” Matendo 8:36.

**Ili ambatize towashi Philipo alimchukua wapi?**

“Akaamuru lile gari lisimame wakateremka wote wawili majini, Filipo na yule Towashi; naye akabatizwa.” Fungu la 38.

**Mwanzo wa kuhubiri kazi ya Mungu alitoa mfano gani ambao ulikuwa faida kwa wafuasi wake?**

“Wakati huo Yesu akaja kutoka Galilaya mpaka Yordani kwa Yohana ili abatizwe.” Mathayo 3:13.

## *Kipawa cha Kutoa*

**Ni nini Yesu alisema kuhusu hali ya kubarikiwa kwa kutoa?**

“Katika mambo yote nimewaonyesha ya kuwa kwa kushika kazi hivi imewapasa kuwasaidia wanyonge, na kuyakumbuka maneno ya Bwana Yesu, jinsi alivyosema mwenyewe, ni heri kutoa kuliko kupokea.” Matendo 20:35.

**Ni kufunga kwa aina gani kunakubaliwa na Mungu?**

“Je! saumu niliyochagua, siyo ya namna hii?.... Je! sio kuwagawia wenye njaa chakula chako, na kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako? Umwonapo mtu aliye uchi, mvike nguo; wala usijifiche na mtu mwenye damu moja nawe?” Isaya 58:6-7.

**Ni kwa njia ipi moja ambayo tunahitajika kumtii Mungu?**

“Mheshimu Bwana kwa mali yako, na kwa malimbuko ya mazao yako yote.” Methali 3:9.

**Ni sehemu ipi ya mapato ya mtu Mungu anasema ni yake?**

“Tena zaka yote ya nchi, kama ni mbegu ya nchi, au kama ni matunda ya nchi, ni ya Bwana; ni takatifu kwa Bwana.” Walawi 27:30.

**Ni kutokana na usaidizi wa nani na kwa kazi gani fungu la kumi lilikuwa linatolewa katika Israeli?**

“Na wana wa Lawi, nimewapa zaka yote katika Israeli kuwa urithi wao, badala ya huo utumishi wautumikiao, maana, ni huo utumishi wa hema ya kutokana.” Hesabu 18:21.

**Ni kwa njia gani tumekosa kama hatutoi fungu la kumi na sadaka?**

“Je! mwanadamu atamwibia Mungu? Lakini ninyi mnaniibia mimi. Lakini ninyi mwasema, tumekuibia kwa namna gani? Mmeniibia zaka na dhabihu.” Malaki 3:8.

**Ni kuhusu nini Mungu anasema tumjaribu na ni kwa mashariti yapi ambayo anatoa**

**ahadi ya baraka nyingi?**

"Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, asema Bwana wa Majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la. nami kwa ajili yenu nitamkemea yeye alaye, wala hataharibu mazao ya ardhi yenu; wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake katika mashamba, asema Bwana wa majeshi." Fungu la 10-11.

**Ni kwa moyo upi Mungu anahitaji sisi kutoa?**

"Kila mtu na atende kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa huzuni, wala si kwa lazima; maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo mkunjufu." 2 Wakorintho 9:7.

**Ni nini Yesu amesema kuhusu kutoa?**

"Ni heri kutoa kuliko kupokea." Matendo 20:35.

**Ni kwa msingi upi zawadi zinapokelewa na Mungu?**

"Maana kama nia ipo, hukubaliwa kadiri ya alivyo navyo mtu, si kwa kadri usivyo navyo." 2 Wakorintho 8:12.

**Yesu alitumia wanafunzi wake inje kuhubiri, kuponya wagojwa na kufufua waliokufa ni nini aliwaambia?**

"Mmepata bure, toeni bure." Mathayo 10:8.

## *Afya Nzuri*

**Mtume Yohana alitaka nini kuhusu gayo?**

"Mpenzi naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya yako, kama vile roho yako ifanikiwavyo." 3 Yohana 2.

**Kwa nini afya ya mwili ipate kulindwa?**

"Maana mmenunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu." I Wakorintho 6:20.

**Ni nini mwili wa mkristo unasemwa kuwa?**

"Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe." Fungu la 19.

**Ni vipi tunahitajika kutoa miili yetu kwa Mungu?**

"Nawasihi...Itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu." Warumi 12:1.

**Ni kusudi gani la juu sana ambalo laweza kuzuia mazoeo yetu ya maisha?**

"Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lo lote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu." I Wakorintho 10:31.

**Ni onyo lipi lililotolewa kinyume cha kuwaongoza wengine kwa kutokuwa na kiwango?**

"Ole wake yeye ampaye jirani yake kiko, wewe utiaye sumu yako, na kumlevya pia, ili kutazama uchi wao!" Habakuki 2:15.

**Walevi wataweza kuingia ufalme wa Mungu?**

"Wala wafiraji, wala walawiti.... wala wevi, wala watamanio, wala walevi, wala watukanaji, wala wanyang'anyi." 1 Wakorintho 6:9-10. tazama Ufunuo 21:27.

**Ni nini moja ya matokeo ya dhambi ya kutokuwa na kiwango?**

"Usiwe miongoni mwao wanywao mvinyo; Miongoni mwao walao nyama kwa pupa. Kwa maana mlevi na mlafi huingia umaskini." Methali 23:20-21.

**Ni nini kitasemwa juu ya utumiaji wa tumbako?**

Kwa kuwa na sumu, Tumbako ya thuru kwa hali ya juu.

**Fahamu**-"Tumbako ndiyo ina hila nyingi sana ya sumu vile inayotambuliwa na wenye elimu ya madawa isipokuwa dawa imekufa na haina nguvu." M. Orfila. Mkuu wa chuo cha mafunzo cha madawa cha Paris.

**Chakula cha kwanza kilipeanwa kwa mwanadamu ni kipi?**

"Mungu akasema, tazama, nimewapa kila mche utoao mbegu, ulio juu ya uso wa nchi yote pia, na kila mti, ambao matunda yake yana mbegu; vitakuwa ndivyo chakula chenu." Mwanzo 1:29.

**Fahamu**-Kwa vingine mboga, nafaka, matunda, na njugu.

**Wakati Mungu alichagua Waisraeli kuwa watu wake ni aina gani ya nyama iliyotolewa kutoka kwa vyakula vyao kwa njia yamaandiko?**

Wale waitwao najisi: tazama Walawi 11 na Kumbukumbu 14.

## *Wako Wapi Waliokufa*

**Ni kwa njia ipi bibilia inatoa mfano kuhusu kifo?**

"Lakini, ndugu, hatutaki msijue habari zao waliolala mauti, msije mkahuzunika kamwe na wengine wasio na matumaini." I Wathesolonike 4:13. tazama I Wakorintho 15:18,20; Yohana 11:11-14.

"Tena, wengi hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka." Danieli 12:2. Tazama Mhubiri 3:20;9:10.

**Wenye haki waliokufa mbinguni wanamtukuza Mungu?**

"Maana Daudi hakupanda mbinguni." Matendo 2:34. "Sio wafu wamsifuo Bwana wala wo wote washukao kwenye kimya." Zaburi 115:17.

**Mtu anamjua Mungu kiwango kipi akiwa amekufa?**

"Maana mautini hapana kumbukumbu lako." Zaburi 6:5.

**Aliye katika hali hii anajua nini kuhusu familia yake?**

"Wanawe hufikilia heshima, wala yeye hajui; kisha wao huaibishwa, lakini yeye hana habari zao." Ayubu 14:21.

**Ni nini kinafanyika na mafikara ya mwanadamu akiwa amekufa?**

"Pumzi yake hutoka, huurudia udongo wake, siku hiyo mawazo yake yapotea." Zaburi 146:4.

**Waliokufa wanajua kitu?**

"Kwa sababu walio hai wanajua ya kwamba watakufa, lakini wafu hawajui neno lo lote." Mhubiri 9:5.

**Wanajukumu lolote katika mambo ya ulimwengu?**

"Mapenzi yao na machukio yao, na husuda yao, imepotea yote pamoja; wala hawana sehemu tena katika jambo lo lote lililofanyika chini ya jua." Fungu la 6.

**Nilini wema watafufuliwa?**

"Kwa sababu Bwana mwenyewa atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza." 1 Wathesalonike 4:16.

**Ni nini kinakuja kwa binadamu wote kwa sababu ya kuanguka?**

"Kwa Adamu wote hufa." 1 Wakor-itho 15:22. tazama Warumi 5:12

**Ni kiwango kipi tunafanya tukiwa tumekufa?**

"Lo lote mkono wako utakalolipata kulifanya, ulifanye kwa nguvu zako; kwa kuwa hakuna kazi, wala shauri, wala maarifa, wala hekima, huko kuzimu uendako wewe." Mhubiri 9:10.

**Ni sauti ya nani inafufua wafu?**

"Msistaajabie maneno hayo; kwa maana saa yaja, ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu." Yohana 5:28-29.

**Ni kwa njia gani tarumbeta juu ya walikufa na makaburi inaelezewa?**

"Ku wapi, ewe mauti, uchungu wako?" I Wakorintho 15:55.

**Ni kwambatana na mwili wa nani walifufuka wataumbwa?**

"Tunatazamia mwokozi, Bwana Yesu Kristo; atakayeubadili mwili wetu waunyonge, upate kufanana na mwili wake wa utukufu." Wafilipi 3:20-21.

## *Kuanzishwa kwa Sabato*

**Ni lini na ni kupitia kwa nani sabato iliumbwa?**

"Basi mbingu na nchi zikamalizika, na jeshi lake lote. Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi yake yote aliyoifanya; akastarehe siku ya saba, akaacha kufanfa kazi yake yote aliyoifanya." Mwanzo 2:1-2.

"Mungu akaibariki siku ya saba, akaitakasa kwa sababu katika siku hiyo Mungu alistarehe, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoiumba na kuifanya." Mwanzo 2:3.

**Ni kwa nini siku ya sabato inatakiwa kuwa takatifu?**

"Maana kwa siku sita Bwana alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo Bwana akaibariki siku ya sabato akaitakasa." Kutoka 20: 11.

**Fahamu**-Sabato ni ukumbusho wa uumbaji, Mungu alionyesha hivi kwa kulitunza na mwanadamu apaswa kumkumbuka Mungu wa kweli na aliye hai muumbaji wa vitu vyote.

**Ni siku gani ambayo ni sabato?**

"Lakini siku ya saba ni Sabato." Kutoka 20:10.

**Sabato ilikuwa inachukuliwa**

**kuwa siku ya mataifa ya kuabudu?**

"Mtafanya kazi siku sita; lakini siku ya saba ni Sabato ya kustarehe kabisa, kusanyiko takatifu." Walawi 23:3.

**Ni kwa kusudi gani lingine Mungu anasema alitoa kwa watu wake kuwa kama taswira au ukumbusho?**

"Tena naliwapa Sabato zangu, ziwe ishara kati ya mimi na wao, wapate kujua ya kuwa mimi, Bwana, ndimi niwatakasaye." Ezekieli 20:12.

**Ni mara ngapi waliokombolewa watakusanyika kumtukuza Mungu?**

"Kama vile mbingu mpya na nchi mpya, nitakazofanya, zitakavyokaa mbele zangu, asema Bwana, ndivyo uzao wenu na jina lenu litakavyo kaa. Na itakuwa, mwezi mpya hata mwezi mpya, na sabato hata sabato, wanadamu wote watakuja kuabudu mbele zangu, asema Bwana." Isaya 66:22-23.

**Ni lini kulingana na biblia sabato inaanza?**

"Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku moja....Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya pili." Tazama Mwanzo 1:5, 8,13,19, 23,31.

"Tangu jioni hata jioni, mtaishika hiyo Sabato yenu." Walawi 23:32. Tazama Marko 1:32.

**Kristo akiwa ulimwengu alitunza sabato?**

"Siku ya Sabato akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi yake, akasimama ili asome." Luka 4:16.

**Ingawa Mungu muumbaji, na mwanzilishi wa sabato, ni vipi alivyotazamwa na kupelelezwa hata siku za leo?**

"Na waandishi na Mafarisayo walikuwa wakimvizia, ili waone kwamba ataponya siku ya sabato; kusudi wapate neno la kumshitakia." Luka 6:7.

**Ni kwa njia ipi Kristo alikuta maoni yao ya uongo juu ya kutunza kwa sabato?**

"Ndipo yesu akawaambia,... na wauliza ninyi, je! ni halali siku ya Sabato kutenda mema, au kutenda mabaya; kuponya roho au kuangamiza?" Fungu la 9.

"Wakajawa na uchungu, waka-shauriana wao kwa wao wamtendeje Yesu." Fungu la 11.

"Mara wakatoka wale Mafarisayo, wakawa wakifanya shauri juu yake.... jinsi ya kumwangamiza." Marko 3:6.

## *Siku ya Bwana*

**Ni siku ipi Yohana anasema alikuwa katika roho?**

"Nilikuwa katika Roho, siku ya Bwana." Ufunuo 1:10.

**Ni siku ipi sheria inasema ni siku ya Bwana?**

"Siku Ya saba ni Sabato ya Bwana." Kutoka 20:10.

**Isaiah anapoongea kwa niaba ya Mungu huiita siku ya saba nini?**

> **Amri ya nne.**
>
> **"Yenyewe (kanisa katoliki) waliiondoa amri ya nne ya sabato ya Mungu na kutunza jumapili siku ya sherehe. (N. Summerbell, *History of the Christian Church* 1873 p. 415).**
>
> **Jumapili kama siku ya juma iliyotengwa kwa ibada zilizowekwa za Mungu mkuu, itakaswe kwa kutokufanywa kazi yoyote, biashara, shuguli za kidunia na kwa kujitolea, yote ni mipango ya kanisa la katoliki. *American Catholic Quarterly Review*, Janu-ary, 1883, pp. 152,139.**
>
> **"Kama waprotestanti wangefuata bibilia basi wangeabudu Mungu siku ya sabato. kwa kutunza Jumapili wanafuata amri ya kanisa la katoliki." Albert Smith, Chancillor of the Archdi-ocese of Balitmore. replying for the cardinal in a letter of Feb. 10, 1920.**

"siku yangu takatifu." Isaya 58:13.

**Ni siku ipi Yohana awe lazima alikuwa katika Roho?**

Ya saba ama alilenga siku ye yoyote ya juma?

**Fahamu**-Hakuna siku nyingine katika bibilia yote inadaiwa na Mungu kama siku yake.

**Yesu alitunza sabato?**

"siku ya Sabato akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi yake, akasimama ili asome." Luka 4:16. "Kama vile mimi nilivyozishika amri za baba yangu." Yohana 15:10.

**Wafuasi wa Yesu walitunza sabato baada ya kifo chake?**

"Wakarudi, wakafanya tayari manukato na marhamu. Na siku ya Sabato walistarehe kama ilivyoamriwa." Luka 23: 56.

"Ili watu wote waheshimu Mwana kama vile wanavyomheshimu Baba." Yohana 5:23. "Mimi na Baba tu umoja." Yohana 10:30.

**Fahamu**-Mwanadamu hapa anamaanisha wanadamu.

**Ni nini Kristo alisema Mwan-adamu ni bwana wake?**

"Kwa maana Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa Sabato." Mathayo 12:8. Tazama Marko 2:28.

**Nani alifanya sabato?**

"Vyote vilifanyika kwa huyo (Kristo, ambaye ni neno)." Yohana 1:3.

**Ni siku ipi inatangulia siku ya kwanza ya juma?**

"Hata Sabato ilipokwisha, ikapambazuka siku ya kwanza ya juma." Mathayo 28:1.

**Fahamu**-Kulingana na agano jipya basi sabato ilikuwa imepita kulipopambazuka siku ya kwanza ya juma.

**Baada ya kusulubiwa ni siku ipi ilitunzwa na wanawakewaliokuwa wamefuata Yesu?**

"Wakarudi, wakafanya tayari manukato na marhamu. Na siku ya Sabato walistarehe kama ilivyoamriwa." Luka 23: 56.

**Ni siku ipi ya juma iliyo sabato, kulingana na sheria?**

"Lakini siku ya saba ni Sabato ya Mungu "Bwana" wako." Kutoka 20:10.

**Fahamu**-Ni dhahiri basi kwamba sabato ya agano jipya ni sawa na ya agano la kale, na kwamba hakuna agano lolote katika agano jipya lililo tenga siku ya saba ya sabato na kutakasa siku ya kwanza.

**Tofauti na waabudu mnyama, ni vipi waabudu wa Mungu wanavyo elezwa?**

"Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu." Ufunuo 14:12.

## *Badilisho ya Sabato*

**Ni vipi ibada ya Jumapili ilianza?**

Wengi huamini ni Yesu aliyebadilisha sabato, lakini kutokana na maneno yake mwenyewe tunaona hakuja kwa sababu yoyote kama hiyo. Basi jukumu hilo la mageuzi lazima litafutwe mahali pengine.

**Katika hubiri lake linalosifika, Yesu alisema nini kuhusu sheria?**

"Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza." Mathayo 5:17.

"Kwa maana amin, nawaambia, mpaka mbingu na nchi zitakap-oondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka, hata yote yatimie." Fungu la 18.

"Basi mtu yeyote atakayevunja amri moja katika hizi zilizo ndogo, na kuwafundisha watu hivyo, ataitwa mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni." Fungu la 19.

**Kupitia nabii Danieli, nini Mungu alisema "pembe ndogo" na utawala anao usimamia ungeazimia kufanya?**

"Naye atanena maneno kinyume chake aliye juu, naye atawadhoofisha watakatifu wake aliye juu; naye ataazimu kubadili majira na sheria." Danieli 7:25.

**Ni utawala upi unadai jukumu nla kubadilisha amri za Mungu?**

Upapa.

**Je ni mafundisho yapi wana-damu wanayo yafunza badala ya neno hilo la uhai na Roho?**

"Nao waniabudu bure wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu,.... Akawaambia, vema! mwaikataa amri ya Mungu mpate kuyashika mapokeo yenu." Marko 7:7-9.

"Mtasitasita katikati ya mawazo mawili hata lini? Bwana akiwa ndiye Mungu, mfuateni; Bali ikiwa Baali ni mungu, haya! mfuateni yeye." 1 Wafalme 18:21.

## *Ujumbe wa Mungu wa Mwisho kwa Ulimwengu wenye dhambi*

Yesu akasema, "Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja." Mathayo 24:14.

Msomaji, katika jarida hili ndogo unayo injili ya Yesu kristo Kama ilivyo katika Bibilia,bila desturi au philosofia ya wanadamu.

"Akasema kwa suati kuu, Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja. Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji." Ufunuo 14:7.

Hukumu ya Mungu ilianzishwa mbinguni mwaka wa 1844. Ilianza kwa wafu. Wafu hawako mbinguni, wamelala makaburini wakingojea ufufuo. "wengine wapate uzima wa milele wengine aibu na kudharauliwa milele". Danieli 12:2

Hivi karibuni, ukaribu usiojulikana hukumu itaanzishwa kwa walio hai.

"Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji." Ufunuo 14:7.

Mariamu mamake Yesu yu kaburini. Hawezi kusaidia yeyote.

Yesu akasema, "Mimi na Baba tu umoja. Basi Wayahudi wakaokota mawe tena ili wampige. Yesu akawajibu, Kazi njema nyingi nimewaonyesha, zitokazo kwa Baba; kwa ajili ya kazi ipi katika hizo mnanipiga kwa mawe? Wayahudi wakamjibu, Kwa ajili ya kazi njema hatukupigi kwa mawe; bali kwa kukufuru, na kwa sababu wewe uliye mwanadamu wajifanya mwenyewe u Mungu." Yohana 10:30-33.

"Kisha mwingine, malaika wa pili, akafuata, akisema, Umean-guka, umeanguka Babeli." Ufun-uo.14:8.

## *Babeli ni Nani?*

Kitabu cha ufunuo kinachukua majina na mahali na vitu kutoka kwa mambo halisi katika agano la kale kutumia haya majina na vitu kwa mifano katika agano jipya:

Katika ufunuo, Babeli hutumika kumaanisha makanisa yaliyoanguka.

"Maana ndio ulio wanywesha mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake." Ufunuo.14:8.

Belshazza alimpinga Mungu kwa ulevi wake. "Wakanywa divai, wakaisfu miungu ya dhahabu, na ya fedha, na ya shaba, na ya chuma, na ya mti, na ya mawe. Kitabu Cha." Danieli 5:4.

**Hakuna mwanadamu, Papa, Kuhani au Mhubiri anaeweza kusamehe dhambi. Hakuna mwanadamu anayepaswa kuabudiwa. "Ndipo Yesu alipomwambia, Nenda zako, Shetani; kwa maana imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake." Mathayo 4:10.**

"Babeli umekuwa kikombe cha dhahabu mkononi mwa Bwana; kilicholevya dunia yote; mataifa wamekunywa mvinyo wake; kwa sababu hiyo mataifa wameingiwa na wazimu." Yeramia 51:7

**Babeli ni mfano wa dini ya uongo na mvinyo ni mfano wa mafundisho yake.** "Akaja mmoja wa wale malaika saba, wenye vile vitasa saba, akanena nami, akisema, Njoo huku, nitakuonyesha hukumu ya yule kahaba mkuu aketiye juu ya maji mengi; [Kisha akaniambia, Yale maji uliyoyaona, hapo aketipo yule kahaba, ni jamaa na makutano na mataifa na lugha. Ufunuo 17:15] Ambaye wafalme wa nchi wamezini naye,nao wakaao katika nchi wamelevywa kwa mvinyo ya uasherati wake....

Na mwanamke yule alikuwa amevikwa nguo ya rangi ya zambarau, na nyekundu, amepambwa kwa dhahabu, na kito cha thamani, na lulu, naye alikuwa na kikombe cha dhahabu mkononi mwake, kilichojawa na machukizo, na machafu ya uasherati wake

"Na katika kipaji cha uso wake alikuwa na jina limeandikwa, la siri, BABELI MKUU, MAMA WA MAKAHABA NA MACHUKIZO YA NCHI.

"Nikamwoma yule mwanamke amelewa kwa damu ya watakatifu, na kwa damu ya mashahidi wa Yesu." Ufunuo 17 :1-6.

Mwanamke katika unabii ni mfano wa kanisa lililo nzuri au kanisa lililo asi. Mwanamke mwovu (kanisa la uongo) linaitwa kahaba. Tazama Ufunuo 17:1.

Mwanamke mzuri (kanisa la kweli) linaitwa bikira Tazama Ufunuo 14:4. mwanamke mwovu huzini na waflme wa dunia. Tazama Ufunuo 17:2.

Mwanamke mzuri anaolewa na Kristo. Tazama 2 Wakorintho 11:2.

Mwanamke mwovu anavalia zambarau na nyekudu iliyorembeshwa kwa dhahabu na mawe ya dhamani. Tazama Ufunuo 17:4.

Mwanamke mzuri amevalia kitani nzuri kisafi, cheupe. Tazama Ufunuo 19:8. Mwanamke mwovu hufundisha utamadanu na uchafu wa uzinifu wake. Tazama Ufunuo 17:4. Mwanamke mzuri hufundisha neno takatifu la Mungu. Tazama Ufunuo 14:5

Mwanamke mwovu hufanya ulimwengu ulazimishwe katika sheria na maagizo ya mwanadamu. Tazama Ufunuo 13:15Mwanamke mzuri hutunza amri za Mungu. Tazama Ufunuo 14:12

Mwanamke mwovu ataadhibiwa na Mungu Tazama Ufunuo 15:2.

"Baada ya hayo naliona malaika mwingine, akishuka kutoka mbinguni, mwenye mamlaka kuu; na nchi ikaangazwa kwa utukufu wake. Akalia kwa sauti kuu, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli ule mkuu; umekuwa maskani ya mashetani, na ngome ya kila roho mchafu, na ngome ya kila ndege mchafu mwenye kuchukiza; Kwa kuwa mataifa yote wamekunywa mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake, na wafalme wa nchi wamezini naye , na wafanya wa nchi wamepata mali kwa nguvu za kiburi chake. Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni, ikisema, Tokeni kwake, enyi watu wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake. Ufunuo 18:1-4.Kutoka katika Babeli ni kutoka katika Makanisa yaliyoanguka.

Na mwingine, malaika wa tatu, akawafuata, akisena kwa sauti kuu, Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama. Ufunuo 14 :9.

## *Mnyama ni nani?*

Nabii Danieli aliona maono na ndoto, "Ndipo wanyama wakubwa wanne wakatoka [baharini, wote wa namna mbalimbali]. "Wa kwanza alikuwa kama simba." Danieli 7:3-4.

Babeli ilitawala ulimw-engu kutoka 606-539 B.C.

"Na tazama, mnyama mwingine.... kama dubu.... naye aliinuliwa upande mmoja." Danieli 7:5.

Sehemu moja ilizidi nguvu sehemu nyingine, Waamedi na Waajemi walitawala ulimwengu kutoka 539 - 331 B.C. Waajemi walikuwa na nguvun zaidi na walitokea nyumaye.

"Tazama.... mwingine, kama chui." Danieli 7: 6. Wayunani walitawla ulimwengu kutoka 331-168 B.C. Tazama, mnyama wa nne, mwenye kutisha, mwenye nguvu, mwenye uwezo mwingi, naya alikuwa na meno ya chuma, na kuyakanyaga mabaki kwa miguu yake; na umbo lake lilikuwa mbali kabisa na wale wa kwanza, naye alikuwa na pembe kumi. Daniali 7:7. Rumi ilitawala kuanzia 168 - 538 A.D.

"Akanena hivi, Huyo mnyama wa nne atakuwa ni ufalme wa nne juu ya dunia." Danieli 7:23. Ufalme wa Rumi uligawanyika katika falme 10 kati ya A.D. 531 na 476.

Nikaziangalia sana pembe zake, na tazama, pembe tatu katika zile za kwanza zikang'olewa kabisa; na tazama, katika pembe hiyo mlikuwa na macho kama macho ya mwanadamu, na kinywa kilichokuwa kikinena maneno makuu. Kitabu cha Danueli 7:8. pembe hii ndogo ni mnyama wa Rev 14:9.

**Upapa.**

Kabla ya kanisa la kipapa kupewa uwezo wote wa kutawala taifa, angeondoa pembe tatu za zile kumi ndogo, Heruli, Vandali, na Ostrogoths. Hizi tawala za kifalme ziliondolewa kabisa kufikia A.D. 538 na kuanzia wakati huu upapa ulikuwa ukitawala wafalme wa dunia kwa mda wa miaka 1260 A.D. 538 hadi 1798. Tazama mchoro.

"Nikatazama, na pembe hiyo hiyo ilifanya vita na watakatifu, ikawashinda; Naye atanena maneno kinyume chake Aliye juu, naye atawadhoofisha watakatifu wake Aliye juu; naye ataazimu kubadili majira na sheria; nao watatiwa mikononi mwake kwa wakati, na

**Mafungu yanayofuata yanatupa china cha kuhesabu nyakati - siku moja sawa na mwaka mmoja.**

**"Kwa hesabu ya hizo siku mlizoipeleleza ile nchi, yaani, siku arobaini kila siku kuhesabiwa mwaka." Hesabu 14:34.**

**Tena utakapozitimiza hizo, utalala kwa ubavu wako wa kuume, nawe utauchukua uovo wa nyumba ya Yuda; siku arobaini, siku moja kwa mwaka mmoja, nimekuagizia. Ezekieli 4:6.**

**"Watatiwa mikononi mwake kwa wakati, na nyakati mbili, na nusu wakati." Kitabu cha Danieli 7:25. Rev 12:14)**

**Wakati - Mwaka mmoja**
**Nyakati - Miaka miwili**
**Nusu nyakati - Nusu mwaka.**

**Kutumia nyakati unabii mwaka mmoja au nyakati = siku 360.**

**Nyakati 3 1/2 = 3 1/2 x 360 = 1260 (siku)**

**Siku moja = mwaka mmoja, 1260 (siku) = 1260 (miaka).**

nyakati mbili, na nusu wakati." Danieli 7 :21,25.

"Wataukanyaga mji mtakatifu [kanisa la kweli] miezi arobaini na miwili." Ufunuo 11 :2.

"Yule mwanamke [kanisa la kweli] akakimbilia nyikani, ambapo ana mahali palipotengenezwa na Mungu, ili wamlishe huko muda wa siku elfu na mia mbili na sitini." Ufunuo 12:6.

Kanisa la kweli liliteswa na kanisa la kirumi kwa miaka 1260, A.D. 538-1798.

## *Mamilioni wauawa*

Kwamba kanisa la Rumi limemwaga damu isiyo na hatia zaidi ya utawala wowote ambao umewahi kuwa katika wanadamu, halitakosolewa na waprotestanti wowote walio na ufahamu mzuri wa historia. Ni vigumu kuwa na ufahamu wa walio naswa na inaeleweka kwamba hakuna uwezo wa kufikiria unaoweza kutibua mateso yao. W.E.H. Leeky, *History of the Rise and Influence of the Spirit of Racialism of Europe* vol. 2:32 1910 Edition.

Kipengele cha maandishi ingawa kirefu kina ufasaha unaoelezea kwa undani haki ya kikatoliki katika, *Catholic Encyclopaedia* vol. 12 :266.

"Kwa kutangaza msimamo wa imani ulio kinyume na mafundisho ya kanisa la Kirumi, Historia hurekodi kuuawa kwa zaidi ya watu milioni mia moja. Millioni moja ya waprotestani (wa swisi na wafaranza) waliangamia wakati wa pigano lililo tangazwa na papa Inocent III mwaka wa 1208. Kuanzia kuimarishwa kwa kundi la Jesuit 1540 -1580 watu mia tisa elfu waliangamia mia moja na hamsini elfu waliangamia kwa kipindi cha miaka dheladhini wakihojiwa, kwa kipindi cha miaka dheladhini na nane baada ya taarifa ya Charles V dhidi ya waprotestanti, hamsini elfu kunyongwa au kukatwa vichwa au kuchomwa moto wakiwa hai. wapinzani wa dini elfu kumi na nane zaidi waliangamia katika uongozi wa Duke Alva wa miaka mitano na nusu." *Brief Bible Readings*, p. 16.

John Wycliff, mtu mwenye uwezo wa Mungu aliaibishwa na mapapa kiasi kwamba miaka 40 baada ya kifo chake mifupa yake ilichimbuliwa tena na kuchomwa hadharani. Ni kupitia kwa maandishi yake Wycliff ambapo makosa mengi ya Kirumi yalipoletwa kwenye mwanga.

Huss na Yerome wote walichomwa hadi kufa wakifungiwa kwa misalaba. Hawangebadilika kutoka kuhubiri ukweli, basi viongozi wa dini wa kikatoliki wakatupwa kwenye moto. (Tazama Wylie, b3, ch 17).

Kuhusu papa Martin Luther aliandika, "ni jambo la kutia hofu kuona mtu ajifanya makamu wa Kristo, akaonyesha, uzuri na utukufu ambao hakuna mfalme anayeweza kufikia. Je hivi ndivyo kuwa kama Yesu aliyekuwa maskini au Petero mnyenyekevu? Yeye ndiye wanasema, Bwana wa ulimwengu; lakini Kristo, ambaye makamu wake anajidai kuwa, alisema hivi. Je uongozi wa makamu waweza kuzidi ule wa mkuu wake?" D'Aubigne, B, Ch.3.

Luther alisema: "na chukizwa na ninapinga (andiko la papa linalomlaani Luther) kama chafu, uongo.... na furahishwa kuvumilia kubeba maumivu kwa ajili ya sababu zilizo njema. Tayari najisikia nina uhuru mwingi ndani ya moyo wangu kwa sababu mwishowe ninajua kwamba papa ndiye mpinga Kristo na enzi yake ni ile ya shetani mwenyewe." D'Aubigne, B.6, Ch 9.

## *Jaribio la kubadili Sabato*

Papa, "ataazimu kubadili sheria na majira." Dan 7:25

"Papa ana uwezo mwingi na nguvu kwamba anaweza kurekebisha na kuelezea au kufafanua hata amri takatifu. Papa anaweza kurekebisha amri takatifu, kwa maana nguvu sio za mwanadamu mbali zile za Mungu na hutumika kama makamu wa Mungu duniani." Lucius Ferraris, *Prompta Bibliotheca*, popa art. 2.

"Kanisa la Rumi hudai kwamba ndio waliogeuza (sabato hadi jumapili) Hawangeota kufanya kitu chochote cha kiroho au kidini bila wao. Na KITENDO HICHO NI ALAMA ya sheria na uwezo wa kidini. James Cardinal Gibbons barua kwa J.F. Snyder wa Bloomigton, Nov. 11, 1895.

SWALI - Je mna njia nyingine yeyote ya kudhihirisha ya kwamba kanisa lina uwezo wa kuweka sherehe za kisheria?

JIBU - "Isingelikuwa na uwezo huo isingefanya yale dini zote za leo zinakubaliana nayo, haingebadilisha sabato, jumamosi hadi jumapili,siku ya kwanza ya juma, badiliko ambalo halina idhini katika maandiko." Priest Stephen Keenan, *A Doctrinal Catechism*, Chap. 2, 174.

"Dhibitisha kwangu kutoka kwa Bibilia yenyewe kwamba yanipasa kutunza jumapilli pekee? Hakuna sheria kama hiyo katika Bibilia. Ni sheria ya kanisa la Kirumi pekee. Bibilia husema,' Ikumbuke siku ya sabato uitakase.' Kanisa la kikatoliki lasema - la! kwa uwezo wa Mungu, na badilisha sabato na ninakuamuru kutunza siku ya kwanza ya juma. Na, tazama, ulimwengu wote unaanguka na kuabudu kwa unyeyekevu kwa agizo la kanisa la katoliki." Priest Thomes Emight, C.S.S.R, President of Redemptionist College, Kansas City, MO. katika hotuba huko Hertrfold, Kansas, Feb. 18, 1884, na katika *American Sentinel*, na katka jarida la Kirumi la June 1839, 173.

Hakuna mwanadamu anayeweza kubadilisha Amri takatifu za Mungu, anafikiria tu anaweza.

Yesu akasema, "Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la sikuja kutangua, bali kutimiliza.

Kwa maana, amin, nawaambia, Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka, hata yote yatimie." Mathayo 5:17 -18.

Paulo aandika, "Mtu awaye yote asiwadanganye kwa njia yo yote; maana haiji, usipokuja kwanza ule ukengeufu; akafunuliwa yule mtu wa kuasi, mwana wa uharibifu; Yule mpingamizi ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa; hata yeye mwenyewe kuketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu." 2 Wathesalonike 2:3-4.

Papa ana heshima ya hali ya juu kiasi kwamba yeye si mwanadamu wa kawaida lakini kana kwamba ni makamu wa Mungu. Papa kwa utukufu hujiona kasoro kuitwa bishop wa mabishop. Yeye pia kiongozi wa Kristo na mfalme wa mfalme. Basi ndio maana anayo taji ya ngazi tatu, kama mfalme wa mbingu na nchi na hata sehemu chini ya ulimwengu." Lucius Ferraris, *Prompta Bibliotheca*, vol. 6, p. 29.

"Nikaona kimoja cha vichwa vyake kana kwamba kimetiwa jeraha la mauti, na pigo lake la mauti likapona. Dunia yote ikamstaajabia mnyama yule." Ufunuo 13:3 "Mtu akichukua mateka atachukuliwa mateka. Mtu akiua kwa upanga, atauawa kwa upanga. Hapa ndipo penye subira na imani ya watakatifu." Ufunuo13 :10.

Tumekwisha onyesha kwamba papa angetawala duniani kwa miaka 1260 kutoka A.D. 538-1798.

Katika 1798 utawala wa mabani uliendelea katika magereza ya ufaranza na jirani ya kikatoliki ikaondolewa nchini Ufaranza chini ya geneari Bathier, aliingia Rumi na kumchukua papa mateka. Tarehe Feb. 10, 1798. "Papa aliyechukuliwa mfungwa alikufa mwaka mmoja baadaye katika Valence, Ufaranza. Kilio kiku kilisikika, "ukatoliki umekufa." upapa ulikuwa umepigwa "jeraha la mauti." Tazama Ufunuo 13:3. Lakini tunaambiwa jeraha lingepona na nyakati zinakuja ambapo "ulimwengu utamfuata mnyama." Tazama ufunuo huo.

1929 Askofu Gaspama alikutana na Premier Mussolini katika ikulu ya St John Lateran mahali mwafaka, ulitiwa saini ya Vatican, Ukiru-dishia upapa uwezo wa mda na ukafanya kuwa utawala ulio na mipaka yake. Lakini jeraha la mauti halijapona kabisa. Jeraha lilikuwa tenganisho la kanisa la Rumi na uwezo juu ya serikali, na jeraha hili litakapopona kabisa kanisa la katoliki litakuwa na uwezo juu ya mahakimu wa serikali. Marekani hakuwa ndio agenti kufanya hayo yatimie.

"Kisha nikaona mnyama mwingine, akipanda juu kutoka katika nchi; naye alikuwa na pembe mbili mfano wa Mwana-Kondoo, akanena kama joka.

Naye atumia uwezo wote wa mnyama yule wa kwanza mbele yake. Naye aifanya dunia na wote wakaao ndani yake wamsujudie mnyama wa kwanza,ambaye jeraha lake la mauti lilipona.." Ufunuo 13:11 -12.

## *Alama ya Mnyama*

"Mtu awaye yote akimsujudu

huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za MwanaKondoo." Ufunuo 14:9-10.

ALAMA YA MNYAMA ni ibada ya JUMAPILI Iliyowekwa kwa Sheria hii ndiyo ALAMA ya Kanisa la Rumi.

Kanisa la katoliki lasema; "kuwa geuzi la [sabato hadi Jumapili] ilikuwa tendo lake.... na tendo hilo ndilo alama ya uwezo wa kidini yake." cardinal Gibbons Nov. 11, 1895)

Marekani hivi karibuni itarudisha uwezo wa upapa.

"Naye awakoseha wale wakaao juu ya nchi, kwa ishara zile alizopewa kuzifanya mbele ya huyo mnyama, akiwaambia wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama, aliyekuwa na jeraha la upanga naye akaishi.

"Akapewa kutia pumzi katika ile sanamu ya mnyama, hata ile sanamu ya mnyama inene, na kuwafanya hao wote wasioisujudu sanamu ya mnyama wauawe.

"Naye awafanya wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa, watiwa chapa katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao;

"Tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile, yaani, jina la mnyama yule, au hesabu ya kibinadamu. Na hesabu yake ni mia sita, sitini na sita. Ufunuo 13:14-17

Marekani ilitokea kimya kimya kutoka ardhini mwaka wa 1798, wakati ule ule upapa ulipoteza uwezo wake. Taifa hili la Marekani liko na pembe mbili kama mwana-kondoo. Taifa bila mfalme na kanisa bila papa. Taifa lililojivunia uhuru wa dini na demokrasia ambapo kila mwananchi ana sauti kwa mambo ya kiserikali. Lakini taifa hili litaongea kama joka.

Katiba ya Marekani inasema, "Bunge haitaweka amri yoyote kuheshimu dini au kuwapiga marufuku wao. Au kupunguza uhuru wa kuongea au wa waandishi au haki ya watu kukutana kwa amani au kulazimisha serikali kusikiliza malalamiko."

Abraham Lincoln katika hotuba yake mjini Gettysburg anasema, "Serekali ya watu, kwa watu, kwa ajili ya watu." Watu wa nchi ya marekani, walitengeneza katiba inayodhamini uhuru wa dini kwa wote. Watu wa marekani, karibuni watabadilika, kwa kura kudai kwamba baraza kuu ya marekani ibadilishe katiba. Bibilia yatueleza kuwa kupitia imani ya kuwa roho (vivuli) za watu waliokufa hurudi na kujionyesha na kuongea na watu dunia nzima itadanganyika. Kutakuwako na dhoruba ya kutisha, mitetemeko ya ardhi, njaa, tauni, na magonjwa. Tunapokaribia mwisho, matukio haya yanazidi mno, kwa hiyo, watu wa mungu watalaumiwa.

**Fikiria mila na desturi hizi za kanisa katoliki miaka ya kuanzisha.**

A.D. 300-Kuombea waliokufa na alama ya msalaba.
321-Sheria za jumapili na kuzingatia utunzaji wa jumapili.
375-Heshima ya malaika na watakatifu waliokufa, na matumizi ya sanamu.
394-Kila siku kusherekea misa ya washenzi na wasio na dini.
400-Mwanzo ya matezo kwa watunza sabato.
431-Kutukuzwa kwa mariamu akiitwa "Mama wa mungu."

450-Adhabu ya kifo kwa watunza wa sabato.
500-Mavazi tofauti kwa makasisi.
526-Kupaka mafuta au utukufu kupita kiasi.
593-Pagatori.
600-Lugha ya kilatini pekee katika maombi na ibada, na maombi kuelekezewa kwa maria, watakatifu waliokufa na malaika.
607-Jina papa au Askofu wa watu wote Dunia Kutumika mara ya kwanza.
709-Kubusu miguu ya papa.
750-Nguvu za kisheria kwa Papa.
786-Kuabudu msalaba, sanamu, mabaki na mifupa ya watakatifu.
850-Maji matakatifu.
927-Chuo cha maaskofu.
965-Ubatizo wa kengele.
995-Kuwapa utawala watakatifu waliokufa katika halmashauri ya kanisa kuu katika majimbo ya maaskofu.
998-kufunga siku ya injumaa na siku ya arobaini alizofunga yesu.
1079- kutoa kwa makasisi.
1090-kutumia rozari na shanga katika maombi.
1184-Kuwa waulizaji.
1190- Uuzanji wa msamaria na hata kabla ya makosa.
1215-Kuomba msamaha wa dhambi kutoka kwa padri au kasisi, na walw si wa mungu.
1220-Kusujudu maji.
1229-Bibilia kupigwa marufuku kusomwa na watu wa kawaida.
1251-Mtulinga.
1414-Kikombe cha divai kupigwa marufuku kwa watu wote isipokua makasisi.
1508-Maombi ya maria kwa kutumia shanga.
1524-Jumuia ya jeshi kuanzishwa.
1545-Mila na desturi kupewa heshima sawa na neno la mungu.
1546- Vitabu vya deuterokanoni kuongezwa katika bibilia.
1854-Dai la kuchukua mimba takatifu.
1864-"Silabi ya upotofu" ya upapa, yapiga marufuku uhuoni wa dini, uhuai wa usemi, haki ya dhamiri, maoneo na mafumbuzi ya utaalamu.
1870-Kuwa papa hawezi kufanya kosa lolote.
1930-Shule za uma, au zozote zisizo za ki-katoliki kuamuliwa kuwa ni bovu.
1950-Kutangazwa kuchukuliwa kwa bikira mariamu mbinguni.
1965-Mariamu kafanywa mama wa kanisa.

Yaongeze haya mengine: kama kiume, wakike, kutoishi na wengine, vyumba pekee ya watawa wa kiume, na pia ya kike, kufunga kwa siku arobaini, wiki takatifu, Jumapili ya matawi, maji matakatifu, Jumatano ya Jivu, siku ya watakatifu wote, siku ya samaki, kupigwa mijeledi, uvumba, mafuta takatifu, nishani, hirizi na mengine mengi.

Walio na imani ya roho za walio kufa pamoja na wahubiri wengine watasema, kwamba matukio haya ya kutisha hayatakoma hadi utukufu wa jumapili uheshimiwa na wote. Watu watadai sheria za jumapili. Marekani itaongoza katika jambo hili, na dunia yote itafuata. " Dunia yote ikamstaajabia mnyama yule." Ufunuo 13:3.

"Naye akawakosesha wale wakaao juu ya nchi kwa ishara zile alizopewa kuzifanya mbele ya yule mnyama, akiwaambia wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama, aliyekuwa na jeraha la upanga naye akaishi". Ufunuo 13:14.

"Wote wanaokataa kutii sheria hii watatishwa na faini, hukumu za kutiwa gerezani na hatimaye kifo.

"Na kuwafanya hao wote wasioisujudu sanamu ya myama wauawe." Ufunuo 13:15.

Sheria hizi za jumapili zitapitishwa na nchi ya marekani, kisha kila nchi usoni pa dunia itafuatia-Mexico ya kale, Marekani kusini, India, Asia, Afrika, na Viziwa vyote baharini. Kila mtu duniani kote, atahitajika kufanya uamuzi, iwapo atatii amri za mungu au sheria za wanadamu.

"Na watu wote wakaao juu ya nchi watamsujudu [mnyama], kila ambaye jina lake halikuandikwa katika kitabu cha uzima cha mwana kondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia." Ufunuo 13:8.

"Na moshi wa maumivu yao hupanda juu milele hata milele, wala hawana raha mchana wala usiku, hao wamsujuduo huyo mnyama na sanamu yake, na kila aipokeaye chapa ya jina lake." Ufunuo 14:11

**Tuna weza kuuliza swali: Roma ya upapa iliwezaje kupata nguvu nyingi hivi?**

"Kisha nikaona mnyama (Roma ya upapa) akitoka katika bahari, mwenye pembe kumi, na vichwa saba, na juu ya vichwa vyake majina ya makufuru.

Na mnyama (Roma ya upapa) niliyemwona alikuwa mfano wa chui, na miguu yake ilikuwa kama miguu ya dubu, na kinywa chake kama kinywa cha simba; yule joka (Roma ya Ukafiri) akampa (Roma ya upapa) nguvu zake, na kiti chake cha enzi na uwezo mwingi na dunia yote ikamstaajabia mnyama yule (Roma

ya upapa)." Ufunuo 13:1-3.

"Kuondolewa kwa ukuu katika milki ya Rumi hadi mji wa constantinople katika mwaka wa 330 iliwacha kanisa ya nchi za magharibi huru na nguvu zote, ili kwendesha shirika zake yenyewe. Askofu wa Roma, akiwa katika kiti cha makaisaria kawa mtu mkuu katika nchi za magharibi, punde alifanywa kuwa kiongozi wa siasa vile vile na wa dini (kiroho)." A.C. Flick, *The Rise of the Medievel Church*.". Uk 168.

"Chochote cha kirumi, kibabari, na kiaryani kilichobakia chini ya ulinzi ya Askofu wa Rumi, aliyefanyika mtu mkuu sana baada ya wafalme wengine kuondoka.... Hivi ndivyo kanisa la kirumi ilivyojisukumia katika utawala ya Milki ya kirumi, ambayo kwa asili ni kuendelea kwake; utawala wa kirumi haujaangamia, bali ilipitia mageuzi. Kanisa katoliki ni ya kisiasa na yajiweka kuwa milki ya dunia, kwasababu ni maendeleo tu ya milki ya Rumi. Papa (Pope), anayejiita Mfalme na kuhani mkuu zaidi (Pontifex Maximus) ndiye aliye miliki viti vya makaisaria. "Adolf Harnock, *What is Christianity?* 1903, Uk 269-270.

Kuna wakristo waaminifu kabisa katika kila kanisa, hata katika kanisa ya katoliki wanaomwabudu mungu siku ya Jumapili. Wamekuwa waaminifu kwa nuru yote walioipata. Wamemtumikia mungu kwa unyofu na moyo kabisa. Hivyo, hawajapokea ALAMA YA MNYAMA. Lakini siku JUMAPILI itatunzwa kwa ajili ya sheria , hapo watakaoitii sheria ya wanadamu na kupuuza ya mungu watapokea alama ya mnyama. Watapata mapigo saba ya mwisho.

"Akaenda huyo wa kwanza akakimimina kitasa chake juu ya nchi; pakawa na jipu baya, bovu, juu ya wale watu wenye chapa ya huyo myama, na wale wenye kuisujudu sanamu yake" Ufunuo 16:2

## *Muhuri wa Mungu*

Siyo wote watakao ipokea alama ya mnyama.

"Tena nikaona kitu kama mfano wa bahari ya kioo iliyochangamana na moto, na wale wenye kushinda, watokao kwa yule mnyama, na sanamu yake, na kwa hesabu ya jina lake, walikuwa wamesimama kandokando ya hiyo bahari ya kioo, wenye vinubi ya Mungu." Ufunuo 15:2.

Wale wasioipokea alama ya mnyama watapokea muhuri ya mungu.

"Akisema, msiidhuru nchi wala bahari, wala miti, hata tutakapokwisha kuwatia muhuri watumwa wa mungu wetu juu ya vipaji vya nyuso zao" Ufunuo 7:3

"Ufunge huo ushuhuda, ukatie muhuri sheria kati ya wanafunzi wangu." Isaya 8:16.

Muhuri wa Mungu wadhihirisha JINA, MAmLAKA na MILKI katika sheria zake.

"Ikumbuke siku ya sabato uitakase, siku sita fanya kazi utende mambo yako yote; Lakini siku ya saba ni sabato ya bwana mungu wako. Siku hiyo usifanye kazi yoyote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana kwa siku sita bwana alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote viliyomo, na akastarehe siku ya saba; kwa hiyo Bwana akaibariki siku ya sabato na akaitakasa." Kutoka 31:17

"Zitakaseni Sabato zangu; nazo zitakuwa ishara kati ya mimi na nyinyi, mpate kujua ya kwamba mimi ndimi Bwana Mungu wenu." Ezekieli 20:20.

Sabato ya siku ya saba, ndiyo bado siku takatifu ya mungu, na utiifu wa sheria za mungu ndiyo itakayo kuwa mtihani kwa muhuri wa mungu.

"Nikaona malaika mwingine, akipanda kutoka maawio ya jua.... Akisema, Msiidhuru nchi, waal bahari, Wala miti, hata tutakapo kwisha kuwatia muhuri watumwa wa mungu wetu juu ya vipaji vya nyuso zao." Ufunuo 7:2-3.

"Kama vile nchi mpya na mbingu mpya nitakazofanya, zitakavyokaa mbele zangu, asema Bwana, ndivyo uzao wenu na jina lenu litakavyokaa. Na itakuwa, mwezi mpya hata mwezi mpya, na sabato hata sabato, wanadamu wote watakuja kuabudu mbele zangu, asema Bwana." Isaya 66:22-23.

"Nalikuwa katika Roho, siku ya Bwana;" Ufunuo 1:10

**"Ni nini siku ya Bwana?**

"Akawaambia, mwana wa Adamu ndiye Bwana wa sabato." Luka 6:5.

Siku ya Bwana ni siku ya saba ya wiki siku ya sabato. "Hapa ndipo penye subira ya watakatifu; hao wazishikao amri za mungu na imani ya yesu. "Ufunuo 14:12

Sheria ya jumapili yaonekana ikifanya vita na watu wa mungu.

"Joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za mungu na kuwa na ushuhuda wa yesu, naye akasimama juu ya mchanga wa bahari." Ufunuo 12:17.

"Heri wazifuao nguo zao, wawe na amri kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake." Ufunuo 22:14.

Makanisa mengi pamoja na hali zingine za ibada hawaitii maagizo yote ya Bibilia. Wanachanganya ukweli na ukafiri, mila na desturi ya maagizo ya wanadamu.

"Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu." Mathayo 15:9.

Utunzaji wa Jumapili ni mila ya wanadamu.Inatokana katika ukafiri wa kuabudu jua. Kutokufa kwa roho siyo imani ya Bibilia.

Ubatizo wa watoto wachanga haifundushwi katika Bibilia. Ubatizo wa kunyunyizia maji haimo katika Bibilia.

"Sisi wakatoliki, ndiyo tulioiweka desturi ya kutunza Jumapili badala ya Jumaamosi kama vile tulivyofanya katika kila sehemu ya imani yetu iitwayo mamlaka ya kanisa. Hivyo basi, ninyi mlio waprotestanti hamna mamlaka hata kidogo kwayo, kwakuwa hakuna katika Bibilia agizo lolote la kutunza Jumapili, na ninyi hamkubali kuwa amrisho kwingineko kote. Ninyi pamoja nasi, kwa kweli, tunafuata mila na desturi katika jambo hili, lakini tunafuata tukiamini kuwa ni sehemu ya neno la mungu, na kanisa katoliki kuwa lina uteusi takatifu kuongoza na kufafanua (maan-diko); Mnaifuata kanisa katoliki mkiikana kuwa inawezakukosa na ni uongozi mdanganyifu, ambao kwa wakati mwingi hutangua neno la mungu kwa ajili ya mapokeo." Matayo 15:9 *The Brotherhood of St. Paul*, "The Clifton Tracts" Vol. 4, track 4, p. 15.

"Nivizuri kuwakumbusha wa Presbyterian, kanisa ya Baptist, Methodist na wakristo wengine wote kuwa Bibilia haiungi mkono kuabudiwa Mungu siku ya Jumapili. Jumapili ni sheria ya kanisa katoliki ya Rumi, na wanaoifuata, wanafuata amri ya kanisa katoliki." Jumapili ya makasisi, katika hotuba ilioripotiwa katika Elizabeth N.J. Taarifa ya tarehe 18th Machi 1903.

**WAPROTESTANTI WAKUBALI**

Maaskofu, wasomi wajuu na waandishi maarufu, wote hutunza Jumapili bila wasiwasi wakijua hiyo ni desturi ya kanisa wala siyo neno la Mungu. Wote pia wanatoa ushahidi kuwa sabato ya Bibilia ni siku ya saba ya wiki. (Jumamosi) na siyo Jumapili. Jumapili siyo siku ya Bwana.

**WAPROTESTESTANI WAZUNGUMZA**

**Congregatinalist:** "Ni jambo lililowazi kuwa, kwa msimamo ule wote, na kwa bidii yote ya unyeyekevu tunayotunza naye Jumapili.... hatutunzi Sabato.... Sabato iliwekwa kwa kusudi fulani, agizo takatifu. Hatuwezi kutetea heshima kama hii kwa utunzaji wa Jumapili.... Hakuna hata sentensi moja katika Agano jipya inayopendekeza kuwa tutapata adhabu kwa kuvunja dai la utakatifu wa jumapili" Dr. R.W. Dale "Amri kumi." uk. 106-107.

**Lutheran Free Church:** "kwa kuwa hakuna hata sehemu moja katika maandiko matakatifun, wala shuhuda yeyote kuwa Bwana mwenyewe wala wanafunzi wake kuamuru kuhamishwa kwa Sabato hadi jumapili, basi ni rahisi kujibu swali hili: Ni nani aliye hamisha sabato, na ni nani aliye na haki ya kufanya hivyo." George Sverdrup, "Siku mpya."

**Presbyterian:** "Hakuna neno, au dokezo katika Agano Jipya kuhusu kutofanya kazi katika siku ya Jumapili. utunzaji wa jumatano ya jivu, au kwaresima yote yana msimamo kama ya utunzaji wa jumapili. Kuingia utunzaji wa jumapili, hakuna agizo katika sheria yeyote." Canod eyton, katika "Amari kumi ." Anglican: "Na ni wapi katika maandiko tunaambiwa kuwa tuabudu Jamapili?" "Tunaamriwa

kutunza Sabato wala hatuamuriwi kutunza siku ya kwanza ya juma." Isaak Williams, "Mahubiri dhahiri ya katekisimu." uk. 334, 336.

**Methodist:** "Nikweli kuwa hakuna agizo kuwabatiza watoto wachanga. Vile hakuna agizo kutunza siku ya kwanza ya wiki. Wengi wanaamini kuwa Yesu alibadilisha Sabato hufanya hivyo kwa msingi wa hadithi za uwongo." Amos Binnery, Theological compendium. uk. 180-181.

**Episcopallian:** "Tumefanya mabadiliko kutoka siku ya saba ya wiki hadi siku ya kwanza ya wiki, kutoka siku ya Jumamosi hadi Jumapili, tukitumia nguvu za kanisa takatifu, katoliki, kanisa la mitume wa Kristo. "Askofu Seymour, "kwanini tunatunza Jumapili."

**Baptist:** "Kwangu mimi, haiwezekani kuwa Yesu, katika maria mitutu ya mazungumzo na wanafunzi wake, hasa sana kuhusu swala la Sabato, wakijadili maadili yake, akiitenganisha na mila na destri ya kiyahudi hajawahi kudokeza uhamisho wa siku hiyo. Hata katika siku zake arobaini baada ya ufufuo wake hakuna kitu kama kile kilichofanyika. Wala roho waliopewa kuwafundisha na kuwakumbusha yote hajajishughulisha na swala hili, wala wanafunzi wakiongozwa na roho kuhubiri injili na kuanzisha makanisa, wakitoa mawaidha na kujenga makanisa, wala kuzugumzia au kuuendea jambo hili.

"Kwa kweli najua kuwa Jumapili haijaja kutumiwa katika historia ya kanisa la wakristo wa kwanza kama siku ya dini, kama tunavyojifunza toka kwa mababa wa wakristo na chanzo cha zingine. Lakini ni jambo la huzuni kuwa hija likiwa na alama ya ukafiri, na kupewa jina la Mungu jua, likaigizwa na kutakaswa na upofu wa upapa na kudaiwa kuwa urithi mtakatifu kwa waprotestanti." Dr. E.T. Hiscox, ripoti ya mahubiri iwe katika mkutano wa wachungaji wa kibaptisti, katika jarida la *New York Examiner*, Nov. 16-1893

Tumenukuu mengi kutoka asili ya kikatoliki ambayo imekuwa ndiyo iliyoibadilisha sabato toka jumamosi, siku ya saba ya wiki hadi jumapili, siku ya kwanza ya juma. Wanakubali pia kuwa wao walileta kuabudu jumapili katika ukristo ili watu wote watunze.

Tumenukuu pia kutoka waprotestani na waandishi wakuu, ambao walishuhudia wazi wazi kuwa hakuna katika Agano la kale wala Agano jipya neno hata moja la kuabudu jumapili au utukufu wa jumapili.

Jumapili si takatifu. Jumapili, kama siku ya ibada ilitoka kwa makafiri walio abudu jua.

**"Mbona ninyi nanyi kuihalifu amri ya Mungu kwa ajili ya mapokeo yenu?** ...Enyi wanafiki, ni vema alivyotabiri Isaya kwa habari zenu, akisema, watu hawa huniheshimu kwa midomo, ila mioyo yao iko mbali nami. Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu....

Onyo la mwisho ni kuhusu alama ya mnyama, itakuwa ujumbe kwa dunia nzima. Utasambazwa kwa radio, runinga, na magazeti katika kila nchi duniani. Mungu atampa kila mtu afanye uamuzi wa mwisho, kumtii yeye au maagizo ya wanadamu ambayo ni kinyume na amri za Mungu.

Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni ikisema, Tokeni kwake, enyi watu wangu, msishiriki dhambi zake wala msipokee mapigo yake. Kwa maana dhambi zake zimefika hata mbinguni na Mungu amekumbuka maovu yake.

Mlipeni kama yeye aivyolipa, mkamlipe mara mbili kwa kadiri ya matendo yake. Katika kikombe kile alichokichanganyisha, mchanganyisheni mara dufu.

"Kwa sababu hayo mapigo yake yatakuja katika siku moja, mauti na huzuni, na njaa naye atateketezwa kabisa kwa moto. Kwa maana Bwana Mungu aliyemhukumu ni mwenye nguvu." Ufunuo 18:1-8.

**"Na waliouawa na BWANA siku ile watakuwapo, toka upande mmoja wa dunia hata upande wa pili; hawataliliwa, wala kukusanywa, wala kukusanywa, wala kuzikwa; wata-kuwa samadi juu ya uso wa nchi." Yeremia 25 :33.**

## *Mungu Atawatunza wote Wamwaminio na Kumtii*

"Hutaogopa hofu ya usiku, Wala mshale urukao mchana, Wala tauni ipitayo gizani, Wala uele uharibuo adhuhuri.

"Ijapo watu elfu waanguka ubavuni pako. Naam, kumi elfu mkono wako wa kuume! Hata hivyo hautakukaribia wewe....

"Kwa kuwa Wewe BWANA ndiwe kimbilio langu; Umem-fanya Aliye juu kuwa makao yako. Mabaya hayatakupata wewe, Wala tauni haitaikaribia hema yako." Zaburi 91:5-7. 9-10.

"Baada ya hayo niliona malaika wanne wamesimama katika pembe nne za nchi, wakizizuia pembe nne za nchi, upeppo uzivume juu ya nchi, wala juu ya bahari, wala juu ya mti wowote.

"Nikaona malaika mwingine akipanda kutoka maawio ya jua, mwenye muhuri wa Mungu aliye hai; akawapigia kelele kwa sauti kuu wale malaika wanne waliopewa kuidhuru nchi na bahari, akisema, msiidhuru nchi,

"Wala bahari, wala miti hata tutakapokwisha kuwatia muhuri watumwa wa Mungu wetu juu ya vipaji vya nyuso zao." Ufunuo 7:1-3.

"Hawataona njaa tena, wala hawataona kiu tena, wala jua halitawapiga, wala hari iliyo yote.

"Kwa maana huyo mwana kondoo, aliye katikati ya kiti cha enzi, atawachunga naye atawaongoza kwenye chemichemi za maji yenye uhai, na Mungu atayafuta machozi yote katika macho yao." Ufunuo 7:16-17.

"Njoni watu wangu, ingia wewe ndani ya vyumba vyako, na ufunge mlango nyumba yako ujifiche kitambo kidogo, mpaka ghadhabu hii itakapopita.

"Tena nikaona kitu kama mfano wa bahari ya kioo iliyochangamana na moto, na wale wenye kushinda, watokao kwa yule mnyama, na sanamu yake na kwa hesabu ya jina lake, walikuwa wamesimama kandokando ya hiyo bahari ya kioo, wenye viruki vya Mungu.

"Nao waliimba wimbo wa Musa, mtumwa wa Mungu, na wimbo wa mwanakondoo, wakisema, ni makuu, na ya ajabu matendo yako e bwana Mungu Mwenyezi; ni za haki na za kweli njia zako, Ee mfalme wa mataifa." Ufunuo 15:1-3.

"Joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya uzao wake waliosalia wazishikao amri za Mungu na kuwa na ushuhuda wa Yesu; naye akasimama juu ya mchanga wa bahari." Ufunuo 12:17.

"Wakati huo Mikaeli atasimama, Jemedari mkuu asimamaye upande wa wana wa watu wako; na kutakuwa na wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati huo huo; na wakati huo, watu wako wataokolewa; kila mmoja atakao onekana ameandikwa katika kitabu kile.

"Tena wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wata-amka,... wengine wapate uzima wa milele." Danieli 12:1-2.

Kisha Mfalme atawaambia wale walioko mkono wake wa kuume, Njoni, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; Mathayo 25:34.

## *Upendo Wa Mungu*

**Mungu anatajwa kuwa nini?**

"Mungu ni Upendo." I Yohana 4:8

**Upendo wa Mungu ni kiasi gani kwa dunia?**

"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." Yohana 3:16.

**Ni kwa jinsi gani hasa, upendo wa Mungu umethibitika?**

"Katika hili pendo la Mungu lilionekana kwetu, kwamba Mungu amemtuma mwanawe pekee ulimwenguni, ili tupate uzima kwa yeye. I Yohana 4:9.

**Ni Wangapi wanaopewa mibaraka na Mungu?**

"Maana yeye huangazia jua lake wao na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki." Mathayo 5:45.

**Kwa mtazamo wa upendo mkuu wa Mungu, ni nini tarajio letu?**

"Yeye asiyemwachilia mwanawe mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye?" Warumi 8:32.

**Wa neno lipi moja twaelezwa tabia ya Mungu?**

"Yeye asiyependa hakumjua Mungu, kwa maana Mungu ni upendo." I Yohana 4:8.

**Upendo wa Mungu una uvumilivu kiasi gani kwetu?**

"Bwana alitokea zamani, akisema, Naam, Nimekupenda kwa upendo wa milele." Yeremia 31:3.

**Je, kuna chochote kinachoweza kumtenganisha mtoto wa kweli wa Mungu na Mungu Mwenyewe?**

"Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu." Warumi 8:38-39.

**Kuabudu Makanisa ya nyumbani**

**Jarida hili linawazilisha ujumbe ulimwenguni, na hasa ule wa Kikristo, ya kwamba utakabiriwa na amri ya kilimwengu itakayo kuamrisha wewe kukoma kufanya kazi siku ya Jumapili (Siku ya kwanza ya Juma). Iwapo utafanya hivyo, utupokea muhuri wa kuhofia, alama ya mnyama, kwenye kipaji cha uso wako. Basi na iwapo badala yake utabudu kwa siku ya saba ya Sabato (Jumamosi), ilio kumbukumbu ya uwezo wa wake wa uumbaji jinsi umeelezewa kwenye amri ya nne ilio amri ya ulimwengu wote (Kutoka 20 :8-11) (Mwanzo 2 :1-3), utaupokea muhuri wa kutamanika wa Mungu katika kipaji cha uso wako na upate kukaa naye milele. Mengi ya makanisa yote, wachungaji, na watu pia, sasa wanabadilisha kuelekea neno wazi la Mungu jinzi limedhihirishwa wazi katika jarida hili na wanachukua msimamo dhabiti kwa utiifu kwa amri za Mungu. Baada ya wewe kuwazilisha ujumbe wazi kwa kanisa lako na wakakataa kuchukua hatua hii basi twakuomba popote ulipo sasa ujitenge na babeli (Ufunou18) kwa kuabudia nyumbani kwako. Waalike jamii, marafiki na majirani mpaka utakapokuwa umefanya vikundi vya waumini wanaochangiana pamoja nawe katika misingi hii ili muwe warekebishaji wa daraja kwenye Amri 10 za Mungu. Hivyo basi waweza kudai ahadi za Kristo: Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao. Mathayo 18:20.**

**Watakatifu watamsifu nani mpaka milele?**

"Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu yake,... utukufu na ukuu una yeye hata milele na milele." Ufunuo 1:5-6.

**Yasemekanaje kuhusu huruma na rehema ya Mungu?**

"Lakini wewe, Bwana, U Mungu wa rehema na neema, Mvumilivu, mwingi wa fadhili na kweli." Zaburi 86:15

**Kwa nini kristo alituagiza tuwapende adui zetu?**

"Lakini mimi nawaambia, wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi, ili mpate kuwa wa Baba aliye mbinguni; maana yeye huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki." Mathayo 5:44-45.

## *Saa ya hukumu ya Mungu*

**Ni ujumbe upi wa ajabu unaotwaliwa katika ufunuo 14:7?**

"Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja. Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji." Ufunuo 14:7.

**Lini saa ya hukumu ya Mungu?**

"Akamwambia, hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu, ndipo patakatifu patakapotakaswa." Danieli 8: 14. Tazama Kielezo.

**Fahamu**-Siku ya upatanisho ya wayahudi ilikuwa katika siku ya kumi ya mwezi wa saba, ambapo patakatifu palitakaswa. Siku hii ya upatanisho ilitazamwa na wayahudi kama siku ya hukumu, na ilikuwa, kwa kweli, mfano wa hukumu ya upelelezi kule Mbinguni. Miaka 2300, kulingana na unabii, yafika kutakaswa kwa hekalu ya Mbinguni, au hukumu ya upelelezi. Mfano wa huduma ya hekalu ya taifa la wayahudi, yakamilishwa, kabisa na kazi ya Kristo. Kama vile siku ya upatanisho katika utawanyo wa kwanza ilivyokuwa siku ya hukumu kweli, vivyo hivyo na upatanisho wa Kristoutahusisha upelelezi wa kesi za watu wake kabla ya kurudi kwake mara ya pili kuwapokea walio wake.

**Ni hakikisho lipi tutakuwa nalo kuwa kutakuwa na hukumu?**

"Mungu...ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki" Matendo 17:30 -31.

**Hukumu ilikuwa ingali katika siku ijayo wakati wa Paulo?**

"Na Paulo alipokuwa akitoa hoja zake katika habari ya haki, na kuwa na kiasi, na hukumu itakayokuja, Felix akafanya hofu." Matendo 24:25.

**Wote watahukumiwa katika mambo gani?**

"Na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao." Ufunuo 20:12.

"Mcheni Mungu, na kumtukuza kwa maana saa ya hukumu yake imekuja." Ufunuo 14:7.

**Je Kristo kama wakili, wa watu wake ana ungama nini mbele ya Baba na malaika wake?**

"Yeye ashindaye atavikwa hayo mavazi meupe, wala sitalivuta jina lake katika kitabu cha uzima, nami tubu jina lake mbele za Baba yangu, na mbele ya malaika wake." Ufunuo 3:5. Tazama Mathtayo 10:32-33, Marko 8:38.

**Fahamu**-Wakati wa hukumu hii, watakatifu na waovu walikufa wangali makaburini. Lakini kumbukumbu la kila mmoja limeandikwa katika vitabu vya mbinguni.

## *Kuja Kwa Kristo Mara Ya Pili*

**Kristo aliahidi nini kuhusu kuja kwake mara ya pili?**

"Msifadhaike mioyoni mwenu, mnamwamini Mungu, niaminini na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi, kama sivyo, ningaliwaambia, maana naenda kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi nayi mwepo." Yohana 14:1-3

**Dalili za kuja kwake zafuatwa na nini?**

"Hapo ndipo watakapommwona mwana wa Adamu akija katika wingu pamoja na nguvu na utukufu mwingi." Luka 21:27.

**Je, kuzungumzia amani duniani kutaleta ulinzi wa uongo?**

"Mlijue kwanza neno hili ya kwamba katika siku za mwisho watakuja na dhihaka zao watu wenye kudhihaki, wafuatao tamaa zao wenyewe, na kusema, imo wapi ahadi ile ya kuja kwake? kwa maana tangu mwanzo wa kuumba. "Petro 3:3-4


**Fahamu-Kuna sehemu tatu katika hukumu inayoelezewa katika maandiko. Hukumu ya upelelezi, kabla ya kurudi kwa Yesu mara ya pili; Hukumu ya dunia iliyopotea na Malaika waovu ambayo itafanywa na Kristo na watakatifu katika zile miaka elfu moja; Na hukumu ya mwisho, adhabu ya waovu wa mwisho wa wakati huo. Hukumu ya upelelezi yafanyika mbinguni kabla Krissto kurundi mara ya pili, ili kuthibitisha wanaostahili ufufuo wa kwanza, atakapokuja, na ni nani kati ya walio hai wanaostahili kugeuzwa miili katika kufumba na kufumbua macho, parapanda ya mwisho itakapolia. Hii ni muhimu kufanyika kabla kurudi kwake mara ya pili kwa kuwa kutakuwa hakuna wakati wa kazi hiyo kati ya kuja kwake na ufufuo wa watakatifu waliokufa. Na hukumu ya mwisho itafanyika watakatifu wameshachungwa hukumu zote wakati ule wa miaka elfu moja. Tazama Ufunuo 20:4-5. 1 Wakorintho 6:1-3. hukumu ya upelelezi ndiyo inatangazwa na ujumbe wa malaika wa." Ufunuo 14:6-7.**

"Maana ninyi wenyewe mnajua yakini ya kuwa siku ya Bwana yaja kama vile mwizi ajavyo usiku. Wakati wasemapo, kuna amani na salama, ndipo uharibifu uwajiapo kwa ghafla,... Bali ninyi ndugu hamumo gizani hata siku ile iwapate kama mwizi." I Wakorintho 5:2-4.

**Katika kupaa kwake, Kristo aliahidi nini kuhusu kurudi kwake?**

"Walipokuwa wakitazamo mbingu yeye alipokuwa akienda zake, tazama, watu wawili wakasimama karibu nao, wenye nguo nyeupe, wasema, enyi watu wa Galilaya mbona mmesimama mkitazama mbinguni? huyu Yesu aliye chukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi hivyo hivyo mlivyo mwona akienda zake mbinguni." Mitume 1:10-11.

**Je, wakati wa dunia wote watajiandaa kukutana naye?**




Zile Miaka 2300 ilikua itufikishe ''tangu kuwekwa amri ya kutengenezwa na kuujenga upya Yerusalemu,'' hadi wakati patakatifu patakapotakaswa.

**Mwaka wa 457 kabla kristo** - Artexerxes, mfalme wa Pashia, aliamuru kuutengeneza na kuujenga upya Yerusalemu.(Danieli 9:24, Ezra 6:1,6-12).Mwanzo wa miaka 2300.

**Mwaka wa 408 kabla Kristo -** kuutengeneza na kuujenga upya Yerusalemu ilimalizika katika mda wa miaka 49 toka kwa unabii mrefu wa Danieli. Kazi hiyo ilimalizika mwaka wa 408 kabla kristo (Danieli 9:25).

**Mwaka wa 27** - akipakwa mafuta na Roho Mtakatifu katika ubatizo wake, alianza kuhubiri. Tazama Mathayo 3:16; Matendo 10:38. Kutoka mwaka wa 457 kabla Kristo hadi "Kupakwa mafuta," ni miaka 483.

"Tazama, yuaja na mawingu; na kila jicho litamwona na hao waliomchoma; na kabila zote za dunia wataomboleza kwa ajili yake." Ufunuo 1:7. "Na wafalme wa dunia, na wakuu wa majemedari, muungwana na matajiri na wenye nguvu na kila mtumwa...wakiiambia milima na miamba tuangukieni, tusizini mbele ya uso wake aketiye juu ya kiti cha enzi na hasira ya mwana kondoo." Ufunuo 6:15-16.

**Kuja kwa Kristo kutakuwa wakati wa malipo?**

"Kwa sababu mwana wa Adamu atakuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika wake; ndipo atakapomlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake." Mathayo 16:27 "Tazama naja upesi na ujira wangu pamoja nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo." Ufunuo 22:12

**Ni kwa nani wokovu umeahidiwa katika kutoka akwa Kristo?**

"Kadhalika Kristo naye, akisha kutolewa sadaka mara moja azichukue dhambi za watu wengi; atatolea mara ya pili, pasipo dhambi, kwa hao wamtazamiao wa wokovu." Waebrania 9:28.

**Ni ushawishi upi imani hii inayo katika maisha?**

Twajua ya kwamba atakapodhihirishwa, tutafanana naye, kwa maana tutamwona kama alivyo. Na kila mwenye matumaini haya katika yeye hujitakaza kama yeye alivyo mtakatifu." Yohana 3:2-3.

**Paulo alitarajia lini taji yake?**

"Baada ya hayo nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana mhukumu mwenye haki, atanipa siku ile wala si tu bali na watu wote pia punde kufunuliwa kwake." II Timotheo 4:8.

## *Jinsi Kristo Atakavyokuja*

Katika kupaa kwake, malaika walisema Kristo atarejea jinsi gani?

"Akisha kusema hayo, walipokuwa wakitazama akainuliwa wingu linampokea kutoka machoni pao. Walipokuwa wakitazama macho mbinguni, yeye alipokuwa akienda zake, tazama watu wawili wakasimama karibu nao, wenye nguo nyeupe, wanasema. Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomuona akienda zake mbinguni." Matendo 1:9-11

**Kristo mwenyewe alisema atakuja jinsi gani?**

"Ndipo itakopoonekana ishara yake mwana wa Adamu mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi. "Mathayo 24:30.

**Onyo la kristo kuhusu maoni ya uwongo ni nini?**

"Wakati huo mtu akiwaambia, tazama, Kristo yupo hapa au yuko kule msisadiki. Kwa maana watatokea wakristo wa uwongo, na manabii wa uwongo nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini hata wateule. Tazama nimekwisha kuwaambia mbele, basi wakiwaambia yumo jangwani, msitoke, yumo nyumbani msisadiki." Mathayo 24:23-26.

**Kwani kuja kwake kutaonekana je?**

"Kwa maana kama vile umeme utokavyo mashariki ukaonekana hata magharibi, hivyo ndivyo utakavyokuwa kuja kwake mwana wa Adamu." Mathayo 24:27. "Ndipo itakapoonkana ishara yake Mwana wa Adamu mbinguni; ndipo mataifa yote ya ulimwengu watakapoomboleza, nao watamewona Mwana wa Adamu akiji juu ya mawingu ya mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi." Mathayo 24:30.

**Nini itafunjwa parapanda itakapolia?**

"Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni na mwaliko na sauti ya malaika mkuu na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza." 1 Wathesalonike 4:16.

**Ni ubaguzi upi mkuu utakapokuwa?**

"Hapo atakapokuja mwana wa Adamu katika utukufu wake, na malaika watakatifu wote pamoja naye, ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu wake, na mataifa yote watakusanyika mbele zake; naye atawabagua kama vile mchungaji abaguavyo kondoo na mbuzi." Mathayo 24:31-32.

**Atawaambiaje walio katika mkono wa kuume?**

Kisha mfalme atawaambia wale walioko mkono wake we kuume, Njooni mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayaari tangu kuumba ulimwengu." Fungu la 34.

**Atawaambiaje walio katika mkono wa kushoto?**

"Kisha atwaambia na wale walioko mkono wa kushoto , Ondokeni kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewaa tayaari Ibilisi na malaika zake." Fungu la 41.

**Bwana atakuwa nini kwa watu wake?**




**Mwaka wa 31** - "Mashili akakatiliwa mbali katikati ya wiki," Mwaka wa 31baada ya kristo, Miaka mitatu na nusu ya kazi ya mibaraka. Tazama Danieli 9:27; Mathayo 27:50-51. Miaka mitatu na nusu iliyosalio ya wiki ya Sabini yatufikisha mwisho wa miaka Sabini iliyotengwa kwa taifa la Wayahudi.

**Mwaka wa 34** - baada Kristo, Stephano Kapigwa mawe. Kutoka wakati hao, injili ilihubiriwa kwa mataifa. TazamaDanieli 9:24; Matendo 7:54-58, 8:1. Kutoka mwaka wa 457 kabla Kristo, hadi wakati wa mataifa ni miaka 490, au wiki Sabini.

**Mwaka wa 1844** - Ujumbe wa malaika watatu wa Ufunuo 14:6-12, ulitoa onyo kwa ulimwengu wote kuhusu kuja kwa Kristo mara ya pili.

**Mwaka wa 1844** - Mwisho wa miaka 2300, kutakaswa patakatifu na hakumu Mbinguni katika saa ya hukumu ya Mungu. Tazama Danieli 8:14; Ufunuo 14:7.

"Naye Bwana atanguruma toka sayuni atatoa sauti yake toka Yerusalemu, na mbinguni na nchi zitatetemeka; lakini Bwana atakuwa kimbilio la watu wake, na ngome ya wana wa Israeli." Yoeli 3:16. Tazama Yeremia 25:30-31, Hagai 2:21, Waebra-nia 12:26, Zaburi 91:5-10.

**Paulo yualezeaje kuja kwake?**

"Kadhalika Kristo naye, akiisha kutolewa sadaka mara moja azichukue dhambi za watu wengi, atatolea mara ya pili, pasipo dhambi, kwa hao wamtazamiao kwa wokovu." Waebrania 9:28.

**Fungu lipi linaloelezea zile miaka elfu moja?**

"Kisha nikaona viti vya enzi, wanaketi juu yake, nao wakapewa hukumu.....wakatawala pamoja na Kristo miaka elfu." Ufunuo 20:4

**Nini watapata waovu wanaoishi Kristo ajapo?**

"Na kama ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika siku zake mwana wa Adamu. Walikuwa wakila na kunywa, walikuwa wakioa na kuolewa, hata siku ile Nuhu alipoingia katika safina gharika ikashuka ikawaangamiza wote. Na kadhalika, kama ilivyokuwa siku za Lutu, walikuwa wakila na kunywa, walikuwa wakinunua na kuuza, wakipanda na kujenga. Lakini siku ile Lutu aliyotoka Sodoma kulikuja moto na kibiriti kutoka mbinguni ikawaangamiza wote. Hivyo ndivyo itakavyokuwa siku ile atakayofunuliwa Mwana wa Adamu." Luka 17:26-30.

## *Miaka Elfu Yaanza*

**Kutakuwa na ufufuo mara ngapi?**

"Msistaajabie maneno hayo; kwa maana saa yaja, ambayo watu wote waliyomo makaburini wataisikia sauti yake, nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu." Yohana 5:28-29

**Ni kundi lipi pekee lina sehemu katika ufufuo wa kwanza?**

Huo ndio ufufuo wa kwanza. Heri, na mtakatifu, ni yeye aliye na sehemu katika ufufuo wa kwanza; juu ya hayo mauti ya pili haina nguvu; bali watakuwa makuhani wa Mungu na wa Kristo, nao watatawala pamoja naye hiyo miaka elfu." Ufunuo 20:6

**Shetani atawekwa gerezani kwa mda mgani?**

"Kisha nikaona malaika akishuka kutoka mbinguni mwenye ufunguo wa kuzimu, na mnyororo mkubwa mkononi mwake. Akashika yule joka wa zamani, ambaye ni ibilisi na shetani, akamfunga miaka elfu; akamtupa katika kuzimu, akamfunga, akatia muhuri juu yake, asipate kuwadanganya mataifa tena. Hata ile miaka elfu itimie; na baada ya hayo yapasa afunguliwe muda mchache."

## Mwanzo wa miaka elfu

1. Mwisho wa mapigo saba ya mwisho.
2. Kuja kwa kristo mara ya pili.
3. Wafu watakatifu wafufuliwa.
4. Wafu waovu kuuawa na shetani kufungwa.
5. Watakatifu wapaa mbinguni.

## Mwisho wa miaka elfu.

1. Kristo na watakatifu washuka.
2. Mji mtakatifu yashuka.
3. Wafu waovu wafufuliwa.
4. Shetani kafunguliwa.
5. Waofu waangamizwa.

Miaka elfu hii, ni mwisho wa wiki kuu ya wakati. Sabato kuu ya miaka 1000 ya histonia ya ulimwengu kwa watu wa Mungu; Takribani miaka 6000 kwa histonia ya ulimwengu.

Kilele cha kufunga injili kwa dunia, na inatangulia mwanzo wa kusimanishwa kwa ufalme wa Mungu duniani.

Yaelezea zaidi wakati unaoitwa katika maandiko, "Siku ya Bwana."

Katika kila uponde, mna ufufuo.

Mwanzo wake unadhihirishwa na kumwagwa kwa mapigo saba ya mwisho, kuja kwa Kristo mara ya pili, ufufuo wa watakatifu, kufungwa kwa shetani, na kubadilishwa miili na kunyakuliwa juu kwa watakatifu hadi mbingu: na mwisho wake, ni kwa kushuka kwa Yesusalemu mpya, pamoja na Kristo na watakatifu, kutoka mbinguni, kufufuliwa kwa waovu, kufuguliwa kwa shetani, na maangamizi ya mwisho kwa waovu.

Katika mda huu wa miaka elfu, dunia yote yawachwa ukiwa : Shetani na Malaika wake wamefungwa hapa, na watakatifu pamoja na kristo wameketi mbinguni wakihukumu waovu kwa maandalio ya adhabu ya mwisho.

# “TAZAMA YUAJA”



Ufunuo 20:1-3.

**Badiliko lipi litafanywa kwa shetani baada ya miaka elfu?**

“Na baada ya hayo yapasa afunguliwe muda mchache.” Ufunuo 20:3.

**Badiliko lipi litafanywa kwa shetani baada ya miaka elfu?**

“Na baada ya hayo yapasa afunguliwe Kristo ajapo. Je, waovu

**Watakatifu waliokufa watafufuliwa kristo ajapo. Je, waovu Waliokufa watafufuliwa lini?**

“Hao wafu waliosalia hawakua hai, hata itimie ile miaka elfu. “Ufunuo 20:5.

**Mara tu waovu wanapofufuliwa shetani atachukuwa hatua gani?**

“Na hiyo miaka elfu itakapokwisha, shetani atafunguliwa, atoke kifungoni mwake’ naye atatoka kuwadanganya mataifa walio katika pembe nne za nchi, gogu na magogu kuwakusanya kwa vita, ambao hesabu yao ni kama mchanga wa bahari.” Ufunuo 20:9

**Kifo chao kitakuwa cha namna gani?**

“Watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele.” 2 Wathesalonike 1:9.

## *Makao ya waliookolewa*

**Dunia iliumbwa kwa kusudi gani?**

“Maana Bwana aliyeziumba mbingu, asema hivi, yeye ni Mungu ndiye aliyeiumba dunia na kuifanya; ndiye aliyeifanya imara; hakuiumba ukiwa, aliiumba ili ikaliwe na watu; Mimi ni Bwana wala hapana mwingine. “ Isaya 45:18.

**Nchi imepewa nani?**

“Mbingu ni mbingu za Bwana, bali nchi amewapa wanadamu.” Zaburi 115:16.

**Mwanadamu aliumbwa kwa kusudi gani?**

“Umemtawaza juu ya kazi za mikono yako; umevitia vitu vyote chini ya miguu yake.” Zaburi 8:6

**Mtu akishindwa huwa mtumwa wa nani?**

“Maana mtu akishindwa na mtu huwa mtumwa wa mtu yule.” 2 Petro 2:19.

**Fahamu**-Mwanadamu alishindwa na shetani kule Edeni hivyo basi akajisalimisha pamoja na mali zake kwa shetani.

**Akimjaribu Yesu, shetani alidai nini kuwa imo mikononi mwake?**

“Akampandisha juu, akamwonyesha milki za ulimwengu kwa dakika moja. Ibilisi akamwambia, nitakupa wewe enzi hii yote na fahari yake kwa kuwa imo mikononi mwangu, nami humpa yeyote kama nipendavyo.” Luka 4:5-6.

**Kwanini Kristo akasema heri wenye upole?**

“Heri wenye upole; maana hao watarithi nchi.” Mathayo 5:5

**Katika jonsi, Yohana alionyeshwa nini?**

“Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya; kwa maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita, wala hapana bahari tena.” Ufunuo 21:1

**Je, mahitaji yao yatatimizwaje?**

“Na itakuwa ya kwamba, kabla hawajaomba, nitajibu na wakiwa katika kunena, nitasikia.” Isaya 65:24

**Je, kutakuwa na amani wakati huo?**

“Mbwa mwitu na mwanakondoo watalisha pamoja, na simba atakula majani kama ng’ombe na mavumbi yatakuwa chakula cha nyoka. Hawatadhuru wala kuharibu katika mlima wangu.

**Ibada itafanywa wakati gani?**

“Kama vile mbingu mpya na nchi mpya, nitakazofanya, zitakavyo-kaa mbele zangu, asema Bwana ndivyo uzao wenu na jina lenu litakavyokaa. Na itakuwa, mwezi mpya hata mwezi mpya na sabato hata sabato, wanadamu wote watakuja kuabudu mbele zangu, asema Bwana.” Isaya 66:22-23.

## *Yerusalem mpya*

**Yohana aliona nini kuhusu mji huu?**

“Nami nikauona mji ule mtakatifu, yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari kama bibi arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe.” Ufunuo 21:2.

**Mji huu una misingi mingapi?**

“Na ukuta wa mji ulikuwa na misingi kumi na miwili, na katika ile misingi majina kumi na mawili ya wale mitume kumi na wawili wa mwanakondoo.” Ufunuo 21:14.

**Ni nini kisichoweza kuingia mji ule?**

“Na ndani yake hakitaingia kamwe chochote kilicho kinyoge. Wala yeye ajaaye machukizo na uongo.” Ufunuo 21:27.

**Ni nini itapita katikati ya mji ule?**

“Kisha akanionyesha mto wa maji ya uzima, wenye kung’aa kama bilauri, ukitoka katika kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwanakondoo.” Ufunuo 22:1.

**Kutakuwa nini katika pande zote za ule mto?**

“Katikati ya njia kuu yake na upande huu na upande huu wa ule mto, ulikuwapo mti wa uzima, uzaao matunda aina kumi na mbili, wenye kutoa matunda yake kila mwezi; na majani ya mti huo ni ya kuwaponya mataifa.” Ufunuo 22:2.

“Njia ya mji ni dhahabu safi kama kioo kiangavu.” Ufunuo 21:21.

**Kwa ni nini mji huu hautahitaji mwangaza wala jua au mwezi?**

“Na mji ule hautahitaji jua wala mwezi kuwangaza, kwa maana utukufu wa Mungu hutia nuru, na taa yake ni mwanakondoo. Na mataifa watatembea katika nuru yake. Na wafalme wa nchi huleta utukufu wao ndani yake.” Ufunuo 21:23-24. Tazama ufunuo 22:5; Isaya 60:19-20.

**Ni nani atakae amriwa kuingia mji ule?**

“Heri wazifuo nguo zao, wawe na amri kuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake.” Ufunuo 22:14. ❑

**“Vita kuu vimekwisha. Dhambi na watenda dhambi hawapo tena. Uumbaji wote ni safi. Ipo maelewano na amani katika uumbaji wote. Kutoka kwake aliyeumba yatiririka uhai, mwanga na furaha na hata kote katika sayuni yote ya angani. Kutoka katika viumbe vidogo sana kupita yote hadi mapana yote ya uumbaji pana amani vitu vyote vijuavyo na visivyojua vyaon-ekana urembo wa ajabu, na furaha, yote yautangaza upendo wa Mungu.” Vita Kuu, uk. 678.**

www.bible-sabbath.com www.earthsfinalwarning.com www.evolution-facts.org
www.present-truth.org www.worldincrisis.org www.pathlights.com www.stepstolife.org

Kijitabu hiki kiliandikwa na:

**Three Angels Ministry**
**P.O. Box 7822 - 00300**
**Nairobi, Kenya**
**Email: markomare@yahoo.com**